ANAYENG'ANG'ANIA

Asante. Mwaweza kuketi, kwa dakika moja. Samahani kwa kuwafanya msimame namna hiyo, lakini walikuwa na kisa cha dharura wakati tu nikiingia, kwa hiyo ilibidi kukishughulikia. "Dharura" ni wakati wanapokuja hapa na inawabidi kurudi. Sisi hujaribu kuwashughulikia mara moja, kwa kuwa hawawezi kukaa.

Nadhani wengi wamekuwa wakishangaa ni kwa nini hatupangi mstari wa maombi papa hapa kuambaa jukwaa. Nina kusudi la kufanya yale ninayofanya. (Mnaona?) Huna budi kupanda mbegu kabla hujapata zao, unaona.

Na halafu, hebu kumbuka tu, shikilia kadi yako ya maombi. Kila mtu aliye na kadi ya maombi. Mtu yeyote anayetaka moja anaweza kupata moja. Mungu akipenda, tutawaombea kabla hatujaondoka kwenye jiji hili. Kama itachukua majuma mawili kuwaombea, tuta—tutawaombea. Kwa hiyo sasa kumbukeni tu, na mshikilie kadi yenu ya maombi, waleteni majirani wenu na wowote wale walio wagonjwa, na hebu wapatieni kadi ya maombi, kusudi waweze kuombewa.

Lakini nina kusudi katika kufanya jambo hili: Kwanza, ni kujenga imani na kupanda mbegu. Na halafu, ukiisha kuelewa, unapokuja kwenye mstari wa maombi, utajua unachojia. Nimeona mengi sana ya hayo yamefanywa katika siku zangu za kuwaombea wagonjwa katika miaka hii kumi na mitano, kumi na minane iliyopita: watu wanakimbia moja kwa moja kwenda jukwaani, wakiwa na, kutoka kwa . . . wakikabiliwa na upasuaji wa dharura, waseme, "Ninajisikia vizuri zaidi, lakini . . ." Na kisha katika siku kadhaa baada ya hapo wanasema, "Nitaninii . . . Nadhani niko afadhali . . ." Nao watafanyiwa upasuaji na hata ha—ha—hata haupo, mnaona, umekwisha. Na wao—wao hawaelewi na jambo hilo, wala hawajui ya kwamba hawana budi kuwa na pi—pingamizi kwa hilo. Na—na wao wananinii tu, hawaelewi.

Mikutano yangu imekuwa ya haraka mno, kuharakisha tu kuingia na kuharakisha kutoka mjini. Moja ya siku hizi, Mungu akipenda na Yesu akikawia, nataka kuja mjini na kukaa muda mrefu kutosha mpaka niweze kuwafanya watu waone kile tunachojaribu kufanya: Ujumbe wa Mungu kwa watu. Niwafundishe siku nzima, asubuhi, alasiri, jioni. Na kuendelea tu kukaa.

Wakati mwingine wakati hawa, tunampata kila mtu (wakati wao wakiwa hawana miamsho katika miji jirani), na kila mhudumu, kusudi apate kuwapeleka waongofu kwa watu . . . kwenye makanisa. Mnaona, mimi sina kanisa, la . . .

Ninawakilisha tu yote hayo, na kujaribu kuwatuma washiriki kwenda, mahali wanakotaka kwenda, hiyo ni juu yao. Jambo muhimu: Je! wamezaliwa mara ya pili? Wanamjua Yesu Kristo kama Mwokozi wao? Basi mwenye hoteli ndiye atakayemchukua kutoka hapo na kuendelea, mnaona. Mungu atampa mamlaka ya kumpeleka jinsi anavyopaswa kwenda. Na ni jukumu langu kuwaelekeza tu kwa Kristo, kuwaombea wagonjwa, kuwamiminia mafuta na kuwapeleka kwa mwenye hoteli. Kwa hiyo basi, wao wanayashughulikia hayo mengine.

Sasa, inaonekana kana kwamba umati wetu umepanuka polepole sana. Sijui tu kama ni ninii . . . Ninakumbuka wakati wa mwisho hapa Kansas, hata tusingepata mahali pakubwa vya kutosha kuwaweka. Kwa hiyo sijui tu: Je!—je! ni wakati ambapo miamsho, tumekuja wakati mbaya? Ama, ni nini, imekuwaje? Ama, watu wamemkataa tu Kristo? Ama, ni kwamba, hawaniamini tena? Ama, sijui ni kitu gani? Ninajua nina ushirikiano mwingi, kwa sababu ninaona kwenye—ninii—ninii—kwenye ratiba na wachungaji wa Assemblies, na Church of God, na makanisa mbalimbali. Nao . . . Jambo fulani lilienda mrama.

Kesho usiku, Bwana akipenda, ningeninii . . . ninataka kuudumisha ujumbe kwa hali rahisi kusudi kila mtu aweze—aweze kufahamu, hata wale . . . wale ambao huenda wasifahamu. Na halafu kesho usiku ninataka kuwa na, takriban, ibada ya namna fulani ya kiinjilisti, kwa ajili ya Jumamosi usiku.

Kesho asubuhi ni Wafanyabiashara wa Full Gospel. Nami ninadhani kuna kundi lao linaloketi hapa. Ni kiamshakinywa chao. Mimi huwahubiria kimataifa. Na kusema kweli, mimi hubeba kadi moja mfukoni mwangu, na hiyo ni ile ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Hao hawana dhehebu. Hiyo ndiyo sababu ninaweza kuchukua kadi yao, ni kwa sababu kwamba siwezi kusema tu, “Mimi ni mfuasi wa Assemblies”; “Mimi ni mfuasi wa United”; “Mimi ni mfuasi wa Church of God”; ama . . . Mnaona, hilo linatupilia mbali ushawishi wote mdogo nilio nao, kwa shirika moja.

Ninaamini watoto wa Mungu wametawanyika kila mahali. Wako—wako kotekote. Na wakati nilipokuja huku kwa mara ya kwanza (bila shaka, mnajua nilikuwa Mbaptisti), na wakati nilipokuja huku miongoni mwa Wapentekoste, wafuasi wa Full Gospel, nikifurahia tukio la kuzaliwa upya, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, kadhalika, niliwazia, “Hilo ndilo lililowafanya Wapentekoste.” Sikujua lilikuwa limejaa ma—madhehebu madogomadogo ya wao wenyewe, lakini wana mengi kadiri Wabaptisti walivyo nayo, kwa hiyo . . . (Ninyi Wabaptisti mnaelewa kuna Wabaptisti wa zamani za kale, walio huru, gandangumu, aina nyingine zote.) Kwa hiyo nikaja huku. Nikawazia, “Ninii tu, ‘Pentekoste,’ inamaanisha kitu kimoja.”

Ningali ninaamini Hilo. Hatuwezi kuiundia Pentekoste dhehebu. Si dhehebu, ni tukio. Mnaona? Hiyo ni kweli.

Kwa hiyo, tuna mashirika madogo, vikundi, na kadhalika. Haitupasi kutofautiana, bali, jinsi wao . . . ni wanadamu tu, nafikiri . . . Nimezungumza na wengi wa viongozi na kadhalika. Sidhani ni miongoni mwa viongozi, nafikiri ni ninii tu, mtu fulani anaingia, anakoroga kitu fulani. Hivyo ni kadiri tu Shetani anavyotaka kufanya, mnaona. Mradi tu mnapigana risasi wenyewe kwa wenyewe, basi hamumpigi yeye risasi. Kama tu tukigeuza nyuso zetu tu, na tuanze kumpiga risasi, lile Kanisa kuu la Mungu aliye hai lingenawiri; Kristo angekuja. Ninaamini hilo. Yeye anatungojea sisi kufanya hivyo. Nami nimejaribu sana niwezavyo, kote katika miaka hii kumi na minane hudumani, kujaribu ku—kuleta hilo pamoja, kuona mioyo yote imeungana kama mmoja, mahema yote yamenyoshwa kuvuka mpaka.

Kama vile Ndugu Grant alivyosema, sio muda mrefu uliopita, huko Texas (nilikuwa nikifanya ibada pamoja naye.), naye akasema, "Ndugu Branham, na—napenda wazo hilo." Kasema, "Unajua, inanikumbusha juu ya jamaa ambaye . . . majirani fulani, wote walikuwa na mabata, na—na kila mmoja wao akawaweka kwenye maskini kijidimbwi kidogo kwenye kitalu cha nyuma, na kukizungushia ua." Akasema, "Vema wajua, ikaanza kunyesha na kunyesha," (Mnajua jinsi Ndugu Grant anavyoweza kuzungumza polepole.) kasema, "kijidimbwi kiliendelea kujaa katika kila kitalu mpaka maji yakapanda juu sana hata yakafurika kupita hizo nyua," kisha kasema, "mabata waliogelea tu kila mahali." Hawakuwa wamezungushiwa ua tena. Kwa hiyo nafikiri kama tunaweza tu kuachilia mkondo wa maji ya baraka za Mungu ujae na kujaa, mnaona, mpaka sisi sote tuwe kwenye kidimbwi kimoja, ama, ziwa lile lile. Hata hivyo, tu mmoja. Ni maskini kanuni ndogo za imani na kadhalika zinazotutenganisha. Lakini tukiwa ni watoto wa Mungu, sote tuko chini ya Familia moja: Mungu.

Mtu mmoja alikuwa na shamba la mahindi wakati mmoja. Mtu mwingine alikuwa na shamba la mahindi. Rubani angeruka juu yake, aseme, "Angalia mahindi ya jamaa huyu, na mahindi ya jamaa yule. Ni mashamba mazuri jinsi gani ya mahindi." Mahindi hayo yaliendelea kukua na kukua mpaka baada ya kitambo kidogo, yakawa juu ya ua, na kufanya shamba moja kubwa la mahindi. Kwa hiyo nafikiri hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Tunaninii tu . . . Kama tukikua kidogo. Lakini mradi tungali wachanga, bado tutakuwa tumefungiwa kwa ua. Lakini tukikomaa, hakutakuwako na tofauti yoyote shambani. Sote tutakuwa shamba moja kubwa. Mungu na atujalie, siku hiyo, kwamba nitaweza kuiona kabla sijaondoka.

Sasa, kumbukeni kesho asubuhi kiamshakinywa cha Wafanya Biashara kitakuwa kwenye . . . Ilikuwa ni Ramada? Ama, [Ndugu mmoja anasema, "Holiday Inn."—Mh.] Holiday

Inn. Ile Holiday Inn. Na kila mtu amealikwa. Nami nafikiri watakuwa na risiti pale, jinsi gani, vyovyote wanavyolifanya. Na Wafanya Biashara wa Full Gospel, kwenu enyi wafanyabiashara, hapa, ni kundi zuri la watu. Na—nawaambia, nafikiri kila mwanamume wa full Gospel anapaswa kuwa mle ndani, kwa ushirika. Ni kweli kabisa. Wana mambo fulani mazuri. Na kama vile nilivyowaambia (ninawahubiria kimataifa), lakini, kila wanapofanya dhehebu kutoka kwake, watakapoanza kujenga ua, ndipo kadi yangu itakaporejeshwa, a-ha, sitaki hilo, mimi . . . halina budi kuwa huru kwa kila mtu.

Kwa hiyo, mnajua Yakobo alichimba kisima, nao Wafilisti wakawafu- . . . wakamfukuza kutoka kwa hicho, naye akakiita "Kijicho." Akachimba kisima kingine, naye akakiita "Ugomvi." Kisha akachimba kingine, akasema, "Ipo nafasi kwetu sote." Kwa hiyo, tunakinywea kisima hicho sasa, ambapo pana nafasi kwa ajili yetu sote, kila mtu.

Sasa, kila mtu anajisikia vizuri? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hilo ni zuri. Hilo, hilo lilisikika kuwa zuri. Ninapenda jambo hilo. Amina, maana yake ni "na iwe hivyo." Mtu fulani . . . Nilikuwa nikihubiri wakati mmoja, kuna mvulana aliyekuwa wa Kanisa la Awali la Baptisti wakati nilipokuwa kwenye Baptisti ya Kimishenari, nami nilikuwa nikihubiri. Kulikuwako na dada mmoja aliyekuwa akiufurahia sana na akaanza kulia na kupaza sauti. Na mwanamume huyu alikuwa mchezaji mzuri kweli wa mpira, naye akakutana nami siku chache baada ya huo. Akasema, "Nilikuja kukusikiliza jana usiku, Billy, lakini," kasema, "nisingeweza kusikia huku hao watu wote kule wakisema, 'Amina.'"

Nikasema, "Loo."

Na akasema, "Mwanamke huyo ameketi pale akilia," kasema, "hilo lilinikera sana."

Nikasema, "Loo, halipaswi kufanya hivyo." Nikasema, "Si—sidhani . . . "

Akasema, "Vema, siwezi kuwazia Mbinguni kukiwa jinsi hiyo."

Nikasema, "Hakika ninaweza."

Akasema, "Vema, hilo lilifanya tu mitetemeko ipitie mgongoni mwangu."

Nikasema, "Kama kweli ungeenda Mbinguni, ungeganda hata ufe, kama ukilisikiliza kundi hilo la kupiga makelele Huko juu. A-ha, a-ha. Wewe ni . . . Hapa ndipo mahali patulivu sana utakapopata kuishi. Nitakwambia jambo hilo. Kwa maana ukienda kuzimu kutakuwako na kulia na kuomboleza na kusaga meno. Kama ukienda Mbinguni, mbona, hata malaika hawakomi, mchana na usiku, kupiga makelele, 'Mtakatifu,

mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi.' Unaona? Mbona, ni chungu nzima ya, 'Haleluya!' na, 'Amina!' na, 'Bwana asifiwe!': vema, hujapata kusikia kama hilo, mpaka utakapousikia ule mkutano Kule juu."

Kwa hiyo, hapa ni mahali panyamavu. Nami daima nilikuwa ninaogopa kitu chochote kinyamavu. Kinasikika kimekufa. Kwa hiyo, mimi—mimi sipendi sana vitu vilivyokufa. Kwa hiyo, chochote kisicho na mhemko kimekufa. Utafiti wa sayansi utathibitisha hilo: chochote kisicho na mhemko. Kwa hiyo kama tukio lako halina mhemko wowote mdogo ndani yake, afadhali uuzike na utafute kitu kilicho na mhemko ndani yake. Hiyo ni kweli. Ni kweli kabisa.

Sasa, sisi sote tunampenda, nina hakika. Bali kuna kupoa kukubwa sana miongoni mwa watu. Uamsho umekwisha. Mioto inazima. Unaona, wakati wa jambo fulani kutukia umewadia. Mwajua, katika hekalu la kale la Kirumi, hekalu la Vesta, wakati mioto ilipozima, kila mtu alienda nyumbani, kwa hiyo hakuna shughuli zilizofanyika. Nafikiri hiyo ni . . . karibu mimi ni mwanachama wa Jamii ya Marafiki kutosha kuamini hilo, ya kwamba—ya kwamba inapaswa kuwa hivyo.

2 Sasa nafikiri, usiku wa leo, nililiruka kila usiku, lakini . . . na—napenda kuliheshimu Neno hili la Mungu, kwa sababu nafikiri ni Neno la Mungu, Nalo ni Yeye. Ni Yeye katika umbo la andiko. Andiko lenyewe, ni, huna budi kuwa na Roho pale wa kulihuisha andiko. Kwa hiyo sasa kwa heshima za Neno hili, hebu na tusimame tunapolisoma. Marko Mtakatifu, mlango wa 7 na kuanzia na kifungu cha 24, na kuendelea kusoma mpaka kifungu cha 30, vyote pamoja. Wewe uliye na Biblia yako, na kwa namna fulani unapenda labda kuchukua fungu dogo la kawaida la kupanda pengine, kwa mbegu chache tena usiku wa leo, kuijenga ile imani mpaka wakati huo utakapofika.

3 Na ninapojisikia ya kwamba Roho ameleta ule upeo, papo hapo kila mmoja wenu ataitwa jukwaani. Msi—msiwe na wasiwasi, mambo yatakuwa sawa wakati huo. Bali mpaka huyo roho atakapofikia mahali hapo hadi mahali ambapo unajisikia ya kwamba watu wamelipata!

4 Kuna haja gani ya kupanda kuja hapa juu, kama unatembea tu kuja hapa? Unapitia kwenye mstari wa Tommy Hicks, na wa Tommy Osborn, na wa Oral Roberts, na huku na huku, kote mstarini. Linaidhoofisha tu imani yako. Hivyo tu.

5 Unapokuja hapa ukiwa na uhakika kabisa ya kwamba hutembei mbele ya ndugu yako, ama mtu yeyote yule, unakuja hapa kwa kuwa Roho wa Mungu ndani yako amekuagiza uje, jambo fulani litatukia. Hakuna kitu cha kulizuia. Mpaka wakati huo, uko tu matembezini, hapa na pale; mhudumu mwingine ajaye mjini, wewe huyu hapa; mhudumu mwingine akija, wewe huyu hapa. Hilo halifai kitu. Hakuna kitu katika mhubiri, si

zaidi ya ilivyo kwa mumeo ama ndugu yako, ama yeyote yule angeweza kuwa. Sisi ni wawakilishi tu Wake, tukiwaambia Neno. Baadhi yao wana karama tofauti, jambo ambalo Biblia inanena juu ya karama hizi. Haya yote yanafanywa kuthibitisha Uwepo Wake.

6 Sasa kama ingelikuwa ni mimi, ama wewe kwangu mimi, kama hamwezi kuaminiana, mbona, hilo lingetosha. Lakini Mungu, mwingi wa rehema, Yeye alituma karama na thibitisho, kuthibitisha, na ili kwamba tu . . . Yeye ni mvumilivu sana, mpole sana na mwema, hata Yeye—Yeye hataki mtu yeyote apotee wala mtu yeyote audhike. Anataka kuhakikisha ya kwamba kila mmoja wenu anaingia. Vema.

7 Sasa mmezifungua Biblia kwenye mlango wa 7 wa Marko Mtakatifu, na kifungu cha 24.

> *Akaondoka huko, akaenda zake hata mipaka ya Tiro na Sidoni. Akaingia katika nyumba, akataka* isininii . . . *akataka isijulikane na mtu; lakini hakuweza kusitirika.*
>
> *Ila mara mwanamke, ambaye binti yake yuna pepo mchafu, alisikia habari zake; akaja akamwangukia miguuni pake.*
>
> *Na yule mwanamke ni Myunani, kabila yake ni Msirofoinike. Akamwomba amtoe pepo katika binti yake.*
>
> *Akamwambia, Waache watoto* washibe *kwanza; maana si vizuri kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia . . . mbwa.*
>
> *Naye akajibu, akamwambia, Naam, Bwana, lakini hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya watoto.*
>
> *Akamwambia, Kwa sababu ya neno hilo, enenda zako, pepo* amemtoka binti yako.
>
> *Akaenda zake nyumbani kwake, akamkuta yule kijana amelazwa kitandani, na yule* pepo amekwisha kumtoka.

8 Sasa hebu na tuombe, na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu. Sijui, tunapoomba, ni wangapi humu ndani wangetaka kukumbukwa katika maombi kwa ajili ya jambo fulani maalumu, ungeinua mkono wako, labda, "Bwana, jalia iwe ni mimi, usiku wa leo" mnaona, ama, "Ninaye mpendwa, jalia iwe ni wao, usiku wa leo."

9 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unazijua haja kabla hata hatujaomba. Yesu alitufundisha kwamba, "Baba yenu anajua mnayohitaji kabla hamjaomba," bali hata hivyo inatupasa kuomba.

10 Wakati alipoangalia mavuno, Yeye alikuwa ni Bwana wa mavuno, Naye alisema, “Mavuno yamekomaa, wafanya kazi ni wachache; ombeni Bwana wa mavuno, apeleke wafanya kazi katika mavuno Yake,” akijifunganisha kabisa na mwanadamu pamoja hata hufanya kazi tu kupitia kwa uwakala wa mwanadamu. Yeye alimchagua mwanadamu apate kumfanyia kazi. Angeliweza kulichagua jua kuihubiri Injili, angelizichagua pepo, ama miti, ama nyota. Lakini alimchagua mwanadamu, akijificha ndani, Yeye hujificha kwa asiyeamini, anajifunua kwa yule ampendaye.

11 Bwana Mungu, tuko hapa usiku wa leo si kwa kusudi lolote lingine bali kukuona Wewe ukijifunua kwetu, kwa kutusamehe dhambi ambazo tumefanya, na—na kutusaidia, na kuwatia moyo watakatifu njiani, kuwaokoa wenye dhambi, kuwaita waliorudi nyuma warejee kwenye ushirika wa Baba wa Mbinguni na kwenye Kanisa la Waaminio, Wazaliwa wa Kwanza. Tujalie, Bwana.

12 Unajua ni nini kilicho nyuma ya kila mmoja wa mikono hiyo iliyoinuliwa juu. Unajua ni nini kilichokuwa chini yake, chini ya huo moyo. Unajua haja zao. Ninaomba dua kwa niaba yao, kwamba utamjalia kila mmoja wao haja zao. Mkono wangu ulikuwa juu, pia, Bwana. Tujalie maombi yetu.

13 Bariki kusomwa kwa Neno Lako. Na sasa tunapolichukua somo, tunaomba ya kwamba Wewe utatufunulia yaliyomo, tupate kumjua Yeye vizuri zaidi. Basi tutakapoondoka hapa, usiku wa leo, jalia tuseme kama wale waliokuwa wakitoka Emau, baada ya Yeye kufufuka katika wafu. Nao walikuwa wametembea pamoja Naye siku nzima, wakazungumza Naye, na hata hivyo hawakujua Yeye alikuwa ni Nani. Wapo wengi kwenye jiji hili, Bwana, usiku wa leo, hapana shaka wamezungumza Nawe na kutembea pamoja Nawe, na hata hivyo kamwe hawakuutambua Uwepo Wako.

14 Lakini usiku ule, wakati Wewe...wakati walipokusihi uingie na kukaa nao, Kleopa na rafiki yake, na wakati ulipoufunga mlango, na ukaketi, ulifanya jambo fulani jinsi tu ulivyolifanya kabla ya kusulibishwa Kwako. Hakuna mwingine, mtu aliyefanya hilo hivyo. Ulilifanya kwa njia Yako Mwenyewe, na, kwa jambo hilo, wakatambua ulikuwa ni Kristo aliyefufuka. Upesi ukatoweka wasikuone tena. Nao wakiwa na moyo mwepesi uliojaa shangwe, upesi waliungana na mitume hao wengine, na wakasema, “Kweli, Yeye amefufuka katika wafu.”

15 Na wakati tunapoondoka kwenye jengo hili, usiku wa leo, jalia tukuone ukijitokeza jukwaani na kufanya mambo yale yale uliyofanya kabla ya kusulibishwa Kwako, kama ulivyoahidi ungerudia tena katika siku za mwisho. Na jalia, Bwana, ya kwamba tutakapoondoka, tutaenda kama wao, tukisema, “Mioyo yetu haikuwaka moto ndani yetu, hapo alipokuwa

akisema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

Mwaweza kuketi.

16 Ningetaka kuchukua Neno moja tu kwa ajili ya fungu, usiku wa leo, nalo neno ninalotaka kuchukua linaitwa: *Anayeng'ang'ania*.

17 Huenda mkasema, "Ndugu Branham, hilo ni—hilo ni neno dogo sana kwa watu mia tatu ama mia nne walioketi hapa usiku wa leo," ama wowote waliopo; mimi si mzuri kwa—kwa—kwa kuikadiria idadi ya wasikilizaji. Nanyi mnasema, "Hilo ni neno dogo sana." Vema, sio ninii—sio ukubwa, ni ninii—ni ninii—ni yale hasa nitakayosema kulihusu.

18 Sasa, *kung'ang'ania*, kulingana na Webster, ni ninii—ni kuwa. . .ni ninii—ni ne—neno, ambalo, unapaswa "kushikilia," pia, linamaanisha kuendelea kushikilia upate kufanikisha lengo fulani, kujaribu ku—kufuatilia kitu fulani, kujaribu kufanya jambo fulani. Wewe ni mng'ang'anizi unaposhikilia.

19 Sasa, Wakristo wote hawana budi kushikilia. Hawana budi kuwa wang'ang'anizi. Na jinsi tu unavyoweza ku—kufanya jambo hili, ni kuwa na imani kwanza katika yale unayojaribu kufanya. Na kama huna imani, unalirukia tu, basi hu—hu—huwezi, huwezi kung'ang'ania. Lakini wakati unapojua kwamba ni ile Kweli, basi hakuna kitu kitakachoweza kukuzuia, wewe kweli unang'ang'ania wakati huo.

20 Na watu wa nyakati zote, ambao wamepata kufanya jambo lolote, na waliokuwa na imani katika yale waliyokuwa wakijaribu kufanya, walikuwa wang'ang'anizi.

21 Kwa mfano, ni kama kwa yule tunayemwita baba wa taifa letu, George Washington. Yeye aling'ang'ania wakati, yeye, akijaribu kupata ushindi dhidi ya Waingereza, naye akauvuka Delaware uliofunikwa na barafu. Aling'ang'ania. Hapakuwapo na kitu. . .Askari wake, nusu yao, hata hawakuwa na viatu miguuni mwao; miguu yao ilikuwa imefunikwa kwa matambara. Upepo ulikuwa ukivuma. Lakini alikuwa ameomba usiku kucha, naye alikuwa na ushindi moyoni mwake. Na hapakuwapo na jeshi la Uingereza wala chochote kile kingemzuia, wala mto uliofunikwa na barafu. Alikuwa ameomba kwa bidii mno, wala hakuna kizuizi kingeliweza kumzuia. Alikuwa mng'ang'anizi, naye akafanikisha jukumu alilokuwa akijaribu ku—kufanikisha, kwa sababu alikuwa na jawabu kutoka kwa Mungu.

22 Mtu anapopata jibu lake kutoka kwa Mungu, hakuna kitu kitakachomzuia.

23 Watu wengi sana leo, kama nitakavyojirudia mwenyewe kutoka usiku wa jana, nikisema wana tumaini badala ya imani. Unapata watu wanaokuja jukwaani, wame—wamejenga tu katika matumaini.

24 “Lakini imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo; ni hakika.” Sio kitu cha kubuni; sio mawazo. Ni kitu ambacho unacho. Unacho tayari. Nawe unakifurahia tu, hiyo imani uliyo nayo, jinsi ungekifurahia kama ungelikuwa na kitu hicho mkononi mwako.

25 Kwa mfano, namna hii, kama ninakufa kwa njaa; na mkate wa boflo unagharimu shilingi ishirini na tano, ambazo zita—zitaununua mkate huo. Sasa, ninapokuwa na shilingi hizo ishirini na tano mkononi mwangu, ninayo furaha tu kana kwamba zilikuwa ni mkate huo wa boflo, kwa maana ndiyo bei ya kuununua mkate huo.

26 Na wakati ninajua moyoni mwangu kwamba nimeikubali, na ninaamini kwamba Mungu amenipa hiyo, nina furaha sana na imani hiyo kadiri ningalikuwa kama niliponywa, kwa sababu nitaponywa, haidhuru. Nina kitu hicho sasa hivi, hakuna mtu anayeweza kuninyang’anya. Ninajua ni kweli, nami ninaweza kuwa mng’ang’anizi na hiyo.

27 Mungu anaposema jambo ambalo litatukia, kama vile maono ama kitu fulani. Nimeona makumi elfu ya hayo, na wengi wenu ni shahidi, wala hakuna moja ya hayo lililopata kushindwa. Na wakati Mungu anaposema jambo lolote, sininii...Kama angesema, usiku wa leo, “Nenda kwenye makaburi ya taifa, kwa kuwa nitamfufua George Washington asubuhi,” ningeualika ulimwengu mzima uje uangalie, litatukia.

28 Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Kamwe Yeye hajawahi kushindwa, wala hawezi kushindwa. Kuna jambo moja ambalo Mungu hawezi kufanya, na hilo ni kushindwa. Hawezi kushindwa. Na Mungu ni Neno Lake.

29 Sasa, Nuhu alikuwa akiishi katika wakati wa kisayansi wakati walipokuwa, labda, wangeweza kuupata mwezi kwa rada. Yesu alisema ilikuwa ni siku kama hii. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

30 Sasa, tunajua, kule Misri tunaziona hizi piramidi. Tusingeweza kuzijenga siku hizi. Hatuna nishati ya kufanya hivyo. Walikuwa wamezishika nguvu za atomiki, ama—ama namna fulani ya nguvu zilizozijenga piramidi. Tusingeweza kuyanyanyua majabali hayo huko juu, kwa njia yoyote. Wala tusingeweza kuyajenga tena yale masfinksi. Hakuna njia ya kufanya hivyo. Hatuna kemikali za kuhifadhi maiti, kuupaka mwili dawa usioze ambapo hata unaonekana uko mzima kwa maelfu ya miaka. Tumeupoteza ustadi huo. Rangi isiyopauka; vitu vingi walivyokuwa navyo wakati huo ambavyo sisi tumefichwa kabisa. Nao walilijenga piramidi hilo linalokaa vizuri sana katikati ya dunia, haidhuru jua liko wapi, kamwe halitoi kivuli, kamwe hakuna kivuli kwenye piramidi. Loo,

ule usanifu wa majengo, vyo—vyo—vyombo wa—walivyokuwa navyo, vimepita vya sasa kwa mbali.

31 Na Nuhu aliishi katika wakati huo wa kielimu, wa kisayansi. Nuhu aliishi katika wakati huo. Naye alikuwa ni nabii, naye Bwana akamwambia ya kwamba kutanyesha. Na baada ya Nuhu kuisikia Sauti ya Mungu, akiwa ni nabii kwa sauti ya Bwana, Neno la Bwana humjia nabii Wake, naye alijua itanyesha; haidhuru mtu mwingine yeyote alisema nini, iwapo ilipata kunyesha.

32 Na haikuwa imenyesha hapo kabla. Mungu aliinyweshea nchi maji, mimea, kwa—kwa umwagiliaji kutoka kwenye chemchemi, na kadhalika, duniani. Kamwe hakukupata kuwa na wingu mbinguni, bali hata hivyo Nuhu alijua maji yangetoka juu. Yeye atafanyaje jambo hilo? Hajui, lakini, aling'ang'ania sana, akatoka akajenga safina kulingana na vipimo kamili ambavyo Mungu alimwambia aijenge, kwa kuwa alikuwa ameisikia sauti ya Mungu, naye alikuwa amesimama Mbele za Mungu wakati sauti ya Mungu ilipodhihirishwa kwake.

Hilo linapaswa kuliwasha moto Kanisa hili lililozaliwa mara ya pili, anayeng'ang'ania!

33 Sijali ni wakosoaji wangapi wanaolicheka, ni wangapi wanaosema haiwezekani, na halafu wanatoka wanaenda huko nje na kulithibitisha kisayansi, wanaupiga picha mwezi kwa rada mwezini na kuonyesha hakuna kitu kama maji angani. Lakini Nuhu alijua ya kwamba kama Mungu, yeye akisimama Mbele Zake, Naye Ndiye Mungu aliyekuwa amenena naye, Naye alitambulishwa kikamilifu ya kwamba lilikuwa ni Neno la Mungu, na akisimama Mbele za Mungu, yeye alikuwa—yeye aling'ang'ania. Angeijenga safina, kwa vyovyote vile; wala hakuna mtu aliyetaka kumsaidia, angeijenga mwenyewe. Yeye aling'ang'ania kwa sababu alijua ya kwamba ilikuwa ni Neno la Mungu, naye akaijenga.

34 Ninaweza kuwazia juu ya—ya jinsi Musa, msomi mashuhuri, alikuwa mwerevu sana hata angeweza—angeweza kuwafundisha Wamisri hekima. Angeweza kuwafundisha waalimu. Alijua the—theolojia yote ambayo Wamisri walijua, na ya familia yake ya Kiebrania. Naye alikuwa ni mtu mwerevu, mwenye akili, nanii mkuu. . .Tunafundishwa ya kwamba alikuwa ni mwanajeshi. Lakini alikuwa ameshindwa kabisa, kwa sababu, jambo moja. Yeye alimwua huyu Mmisri, nayo elimu yake ikakoma; wakati walipomshtaki basi, "Unataka kutuua kama ulivyomwua Mmisri?" Akifikiri ya kwamba ndugu zake wangelielewa hilo. Ndipo a—akashindwa vibaya sana.

35 Na hilo linanileta kwenye wazo la jambo hili. Hiyo ndiyo sababu, usiku wa leo, kwamba mifumo yetu imeshindwa. Hiyo ndiyo sababu kamwe hatutaweza kuwaelimisha watu wamwendee Mungu. Hatutaweza hata kidogo kuwaundia

dhehebu wamwendee Mungu. Tumejaribu mifumo hii yote, nayo yote inashindwa, kama vile, ikaanguka kama ule mnara wa Babeli. Nayo daima itashindwa.

36 Mungu, yule Mungu asiyebadilika, alifanya uamuzi Wake kwenye bustani ya Edeni, jinsi ambavyo angemwokoa mwanadamu.

37 Na wakati Mungu akifanya uamuzi, hauna budi kubaki hivyo daima. Hawezi kubadilika. Hawezi kuwa mwerevu zaidi. Yeye ndiye chanzo cha akili yote. Haidhuru sayansi yetu inasema nini, kama inapingana na ile Akili ama Neno la Mungu, ni kinyume, si sahihi. Sijali inaweza kuthibitishwa kisayansi jinsi gani, ingali si sahihi.

38 Mungu aliamua angemwokoa mwanadamu kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia. Wamejaribu kujenga miji, wamejaribu kuwaunganisha, wamejaribu kujenga minara, kuwaelimisha waingie ndani ya Hilo, nao wanaenda mbali zaidi wakati wote. Kamwe hutaweza kumwokoa mwanadamu mpaka atakapoirudia ile Damu. Hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu atawahi kukutana na mwanadamu. Si kwa akili zake, si kwa jinsi alivyo mwerevu, ni watu wangapi wamemfanya kasisi, ama askofu, ama mzee wa jimbo, ama chochote anachoweza kuwa, mhudumu, shemasi, hapo sipo mahali Mungu anapokutana na mwanadamu. Yeye hukutana Naye mahali hapo wakati anapokuwa chini ya Damu iliyomwagika. Hapo ndipo mahali pekee Israeli walipoweza kukutana na Mungu, kumwabudu, ilikuwa ni chini ya damu iliyomwagika. Hiyo ndiyo njia iliyotolewa na Mungu. Hakuna njia nyingine itakayofanya kazi. Na chini ya Damu iliyomwagika, Mungu hukutana na mwanadamu na kusimama mbele ya mwanadamu.

39 Musa, msomi huyu mtoro, nabii mtoro, huko upande wa nyuma wa jangwa, na kumwoa mwanamke huyu mrembo wa Kushi, naye alikuwa akiishi; alikuwa na mtoto, mtoto Gershomu. Siku moja wakati akitembea huko jangwani, upande wa nyuma wa jangwa, mzee mwenye umri wa miaka themanini, alionekana kana kwamba hakuwa na faida, kama mhudumu, bali aliona kichaka kilichokuwa kikiwaka Moto wala hakikuteketea. Ndipo akasogea kando aone kile kilichokuwa kimetendeka, naye akaingia kwenye Uwepo wa Mungu; na akasikia Uwepo wa Mungu, akasikia sauti ya Mungu, wakati akiwa katika Uwepo Wake, wakati hii Nguzo ya Moto ilipokuwa imekaa kwenye kichaka hiki, ikisema naye. Ambapo, aliogopa hata kwenda karibu na Misri, akijua ya kwamba Farao angeyaondoa maisha yake, hakuna kitu kitakachomzuia sasa.

40 Na wakati mwingine mtu anapoingia katika Uwepo wa Mungu, na kuisikia Sauti ya Mungu, yeye hufanya mambo ya kimapinduzi sa—sana mbali na mawazo ya kawaida ya watu, yanasikika ni ya kipuuzi.

41 Kesho yake sasa. Mtu aliyeogopa kulichukua jeshi kuivamia Misri, watumwa wote kule waliokuwa kule Misri, yeye aliogopa kumshambulia Farao namna hiyo; huyu hapa, kesho yake, umri wa miaka themanini, ndevu zikining'inia kote hadi kiunoni mwake, kichwa chake chenye upara kiking'aa, fimbo iliyopinda mkononi mwake, mkewe ameketi juu ya nyumbu na mtoto nyongani mwake, akishuka kwenda, huku macho yake yameelekezwa juu, akimtukuza Mungu.

"Unaenda wapi, Musa?"

42 "Nashuka kwenda Misri, kuiteka." Uvamizi wa mtu mmoja! Kwa nini? Yeye alikuwa kwenye Uwepo wa Mungu. Aliona yale Mungu angeweza kufanya kwa fimbo. Hakujua yale angelifanya na jeshi. Alijua yale angeweza kufanya na fimbo.

43 Mimi sijui kile anachoweza kufanya na dhehebu. Ninajua kile anachoweza kufanya na mtu mmoja ambaye atajisalimisha mwenyewe kabisa Kwake. Yote anayohitaji, mtu mmoja, huyo ni wewe. Ndipo yeye ni mng'ang'anizi. Hakuna kitu kitakachomzuia.

44 Musa alikuwa ameingia katika Uwepo wa Mungu, akaisikia Sauti Yake katika i—ishara ya kimiujiza. Alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Moto uangamizao, Naye huyu hapa katika Nguzo ya Moto huko nyuma kichakani. Elimu yake yote, theolojia yake yote, ikamwacha. Naye alijua jambo moja: kulikuwako na Mungu, naye alikuwa na maagizo Yake. Fimbo iliyopinda ilikuwa ni nzuri vya kutosha. Alikuwa ameshakuwa katika Uwepo wa Mungu.

45 Haileti tofauti yoyote Misri ilikuwa na watu wangapi waliofunzwa. Lolote la mambo haya halikumaanisha chochote kwa Musa. Alikwisha kuwa katika Uwepo wa Mungu, naye alikuwa mng'ang'anizi. Anashuka kwenda kuiteka, dhidi ya ngao na watu waliofunzwa, kwa makumi elfu, akiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake. Hebu mzuie kama unaweza. Hakuna kitu kinachoweza kumzuia. Naye akafaulu, alishuka akaenda na kuiteka kwa sababu aling'ang'ania wakati alijua yakini kwamba aliisha kuwa katika Uwepo wa Mungu, naye alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu kutoka kwenye Uwepo wa Mungu. Amina. Si kwamba ilikuwa ni sauti tu, bali ilikuwa ni sauti ya Kimaandiko.

Zipo sauti za kila namna. Ichunguze na Neno.

46 Hiyo sauti ilisema, "Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Nilitoa ahadi ya kwamba ningewakomboa watu hao. Wakati huo umewadia. Nimesikia kilio chao, nimeona wanyapara wao wakiwatesa, Nami ninakumbuka ahadi Yangu. Nami nimeshuka kuja kuwakomboa, Nami ninakutuma kufanya hivyo." Hilo ni zuri vya kutosha. Aliuona Utukufu Wake, naye huyoo akaenda.

47 Daudi alikuwa mng'ang'anizi sana wakati alipokuja huku kwenye—kwenye majeshi ya Israeli, ambayo yalikuwa yamesimama kwa tishio wakati huo, na upande wa pili wa kijito hicho kidogo na ng'ambo ya pili walikuwako wa—wale Wafilisti. Kulikuwako na Goliathi, lile jitu lililotoa changamoto, mkubwa na mrefu karibu mara mbili kuliko mtu wa kawaida, vidole vyenye urefu wa inchi kumi na nne; na mkuki mkubwa sana, urefu wa futi kadhaa, ambaye angeweza kusimama pale na kumnyanyua tu mtu kwa huo, namna *hiyo*, na kuwatupilia mbali; awapige na kuwaangusha, awanyanyue kwa mkuki na kuwatupilia mbali, wakikwea kile kilima.

48 Na wakati adui anapojua ya kwamba anakuzidi nguvu, anapenda kujigamba. Kwa hiyo akasema, "Hebu na tusimwage damu nyingi sana." Kasema, "Sauli, acha baadhi ya watu wako waje hapa na kupigana nami. Na kama nikimwua, vema, basi, mtatutumikia. Bali kama akiniua, sisi tutawatumikia." Mnaona, wakati adui anakumudu!

49 Na kila askari alikuwa anatetemeka sana hivi kwamba ilikuwa ni vigumu kushikilia silaha za—zake. Naye Sauli, mtu aliyekuwa na uwezo mwingi kuliko wote, tangu mabega yake kwenda juu kichwani alikuwa ni mrefu kuliko jeshi lake, asingethubutu kumgusa, na hata hivyo alipaswa kuwa ndiye mtiwa mafuta wa Bwana.

50 Lakini kukaja tokea jangwani, maskini jamaa mdogo mwenye mabega yaliyoinama, mwekundu, aliyekuwa na kombeo mkononi mwake. Ndipo jitu hilo likajigamba mbele ya mtu asiyepaswa. Ndipo Daudi akasema, "Mnataka kuniambia ya kwamba mtamwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa kusimama pale na kuyaasi majeshi ya Mungu aliye hai? Unataka kuniambia ya kwamba mtaachilia kitu kama hicho?"

51 Sasa ndugu zake wakasema, "Sasa wewe ni mtundu. Wewe rudi huko nje kwa wanakondoo, ambapo ndipo mahali pako."

52 Ndipo habari zikamfikia Sauli. Sauli akasema, "Mleteni kijana huyo hapa, hebu nimwangalie."

53 Basi wakati alipokuja, maskini jamaa mdogo mwekundu, aliyejikunyata, amesimama pale, labda nywele zikining'inia machoni mwake. Ndipo akasema, "Vema, wewe, wewe huwezi kupigana na mtu yule." Kasema, "Wewe si kitu ila mtu mdogo, mtu m—mdogo mwekundu, na katika ujana wako. Naye amekuwa shujaa tangu ujana wake." Akasema, "Huwezi kupigana naye. Ninapenda ujasiri wako, lakini ninii . . . ni kubwa mno."

54 Ni jambo gani lililotukia? Yeye akasema, "Hebu nione kama ungeweza kuzitumia silaha zangu." Kwa hiyo akamvalisha silaha zake, na kumpa ngao yake.

55 Vema, maskini Daudi mdogo asingeweza kusimama. A—a—akasema ha—hakujua lolote kuhusu hizo. Alikuta kwamba fulana ya Sauli ya kikasisi haikumkaa mtu wa Mungu.

56 Kwa hiyo akasema, "Nitamtuma aende na nikampeleke shuleni kusomea, Ph.D., LL.D., na kadhalika, nione anachoweza kufanya juu ya jambo hilo."

57 Akasema, "Sijui lolote kuhusu vitu hivi. Nivueni hivi. Si—sijui lolote kuhusu hii."

58 "Bali hili hapa jambo moja nijualo. Nilikuwa nikiwachunga kondoo wa baba yangu, ndipo simba akaingia na kumchukua mmoja wao. Nami nikamfuatilia, maana baba yangu alikuwa ameniagiza niwachunge hao kondoo." Amina. Na mchungaji yeyote mzuri ni mwangalizi wa kondoo. Naye akasema, "Sina kitu ila kombeo hili mkononi mwangu, lakini nilimpiga nikamwangusha; na wakati alipoinuka dhidi yangu, nilimuua. Kisha dubu aliingia na kumshika mmoja. Nikamfukuza na kumtoa mdomoni mwake; ndipo alipoinuka, nikamwua." Ndipo kasema, "Ni zaidi sana vipi Mungu wa Israeli, Mungu wa Mbinguni, atamsalimisha huyo Mfilisiti asiyetahiriwa mkononi mwangu!"

59 Maskini jamaa huyo mdogo alikuwa ni mng'ang'anizi kwa kuwa yeye alijua kile alichokuwa akizungumzia. Alimjua Yule aliyekuwa amemwamini, na alikuwa ameshawishika kabisa aliweza kuweka kile alichomkabidhi Yeye kwa ajili ya siku ile. Sasa yeye alikuwa tu na kombeo, hilo tu ndilo alilokuwa nalo. Akasema, "Nitaenda nikapigane na Mfilisti." Kwa sababu, sababu ya yeye kuwa mng'ang'anizi hivi, alijua kama Mungu, katika kuwachunga kondoo, alikuwa amemsaidia kumrejesha yule kondoo kwa baba yake, ni zaidi sana jinsi gani mtu.

60 Sasa wazieni juu ya hilo, wahudumu wote. Nasi tunajisikia namna hiyo kuhusu ninyi kondoo, usiku wa leo. Ibilisi amekuja na kuwapiga kwa ugonjwa. Hiyo ni kweli. Amewaondoa kwenye afya njema. Si—sina Ph.D. Sina LL.D. Sina hata elimu ya sekondari. Bali ninajua kile nilicho nacho. Ninawafuatilia, usiku wa leo, kuwarejesha kwenye kivuli cha malisho ya kijani kibichi na maji matulivu. Hilo ndilo lililotuleta hapa jukwaani, usiku wa leo, ni kuja kuwachukua, kuwanyakua kutoka mkononi mwa simba huko nje, tuwarejeshe. Iweni na subira, sikilizeni kwa makini na mwangalie, jaribuni kujua kile tunachojaribu kufanya, ni kujaribu kuwasaidia.

61 Sasa, Daudi alikuwa mng'ang'anizi sana, kwa sababu kwamba alimjua Yeye aliyemwamini, naye alijua aliweza kuweka, kile kilichowekewa amana, Yeye aliweza kukilinda.

62 Tunaona ya kwamba, Samsoni, mwamuzi mwingine mkuu katika Israeli, na kwamba watu wengine humwona Samsoni kama mtu mwenye ma—mabega yaliyo karibu kufanana na mlango wa ghala; sasa lisingekuwa ni jambo la ajabu kuhusu

hilo, kumwona mtu ambaye angeweza kuyang’oa malango ya Gaza na kuondoka nayo, ama kumnyanyua simba na kumpasua vipande viwili. Lakini, mwajua, Samsoni alikuwa tu ni kananii kadogo tu. . .kwa msemo wa mtaani, maskini kibushuti, kananii kadogo sana, maskini mwenye nywele za kipilipili, dondoandume, mvulana wa mama, vishungi saba. Lilikuwa ni jambo la ajabu. Wakati, walidhani ya kwamba mtu, mtu mkubwa mno wa futi kumi, angeweza kumnyanyua simba, hakika, na kumwua. Lakini jambo la ajabu lilikuwa, jamaa huyu mdogo alionekana hajiwezi mpaka Roho wa Bwana anapokuja juu yake. Haikuwa ni Samsoni. Ilikuwa ni Roho wa Bwana.

63 Hiyo ndiyo sababu haikuwa ni wale mitume. Yesu aliwachagua wote, kila mmoja wao kwa kweli hakuwa hata na elimu ya kuliandika jina lake. Yeye hakuwachagua makasisi. Hakuwachagua wanatheolojia. Aliwachagua wavuvi na wachungaji, wasio na elimu na wasio na maarifa, ili kwamba angeweza kuwachukua hao mikononi Mwake, na kuwachukua wasio na maana na kuwafanya wakawa kitu fulani. Hiyo ndiyo tabia Yake. Kwa hiyo Yeye hazichukui shule zilizofunzwa na wasomi waliofunzwa, Yeye hukichukua kitu kinachotambua ya kwamba si kitu. Yeye huingia ndani yake na kufanya kitu kutoka kwake.

64 Tunaona ya kwamba huyu Samsoni alikuwa ni Mnazarayo, alikuwa na vishungi saba vidogo vilivyoning’inia mgongoni mwake. Ndipo Roho wa Bwana alipomjia, hakuogopa kitu. Kwa nini? Yeye alikuwa mng’ang’anizi mradi tu angeweza kuisikia hiyo nadhiri ya Mnazarayo ikiwa pamoja naye. Mradi tu angeweza kuunyosha mkono wake hapa nyuma na kuvihisi hivyo vishungi, yeye alijua ya kwamba alikuwa katika mapenzi ya Mungu na hakuna kitu kingaliweza kumfunga. Jiji lisingeweza kumfunga. Simba asingeweza kumwua. Alichukua taya la nyumbu, nalo limekauka, na akawaua wafilisti elfu moja, kwa hilo.

65 Je! mnajua helmeti hizo, helmeti hizo za shaba, zilikuwa na unene wa zaidi ya inchi moja? Mnajua ni nini kingetukia wakati maskini mfupa uliokaukia jangwani ungeipiga hiyo? Mbona, ungepasuka ukawa vipande milioni moja. Lakini yeye alisimama pale, peke yake, akiwa na mfupa wa taya la nyumbu, na kuwagonga kichwani mwao, na kuwaua Wafilisti elfu moja. Kwa nini? Aling’ang’ania. Kila alipopiga, aliihisi hiyo nadhiri ya Kinazarayo ikimrudia.

66 Ni kiasi gani kanisa linavyopaswa, usiku wa leo, linalodai ya kwamba mmezaliwa kwa Roho wa Mungu! Kusimama mkutanoni na kuona thibitisho la kufufuka kwa Yesu Kristo, na kudai mmejazwa na Roho Mtakatifu, na mngeketi kimya na kumwacha Shetani awasukume huku na huku kama afanyavyo? Ni jambo la ajabu. Mradi tu unaweza kuuhisi Uwepo wa Roho Mtakatifu, kujua ya kwamba ni Neno Lake na ahadi Yake

kwa siku hii, inakupasa kung'ang'ania ukazane mpaka yote yamekwisha. Anayeng'ang'ania! Kaa nalo! Mungu aliahidi hilo. Si wewe. Ni Mungu!

67 Vipi kuhusu maskini bikira Mariamu. Sasa kwenu ninyi wanawake. Sasa yeye alikuwa ni msichana tu wa kawaida aliyeishi katika mji fisadi sana ulio mbaya kuliko Topeka. Naye aliishi mle, lakini aliishi maisha safi na yaliyonyooka, naye alikuwa ameposwa na mtu jina lake Yusufu. Basi siku moja alikuwa akienda zake kisimani, kuteka maji, ndipo Nuru kuu ikatokea mbele zake. Na Malaika akasimama pale, ambaye alikuwa ni Gabrieli, na akamwambia ya kwamba ata—atamzaa mtoto, pasipo kumjua mwanamume yeyote. Na wakati ule ule, akamwambia kuhusu Elisabeti, bi—binamu yake ambaye alikuwa mkongwe, mke wa Zakaria, naye alikuwa amepata mimba katika siku za uzee wake.

68 Na sasa Mariamu, ungeweza kuwazia ingekuwa ni kichekesho cha namna gani kwa watu, kuwazia ya kwamba maskini msichana huyu mdogo, aliyeambatana na mvulana huyu, kwa uaminifu, na hapa anaonekana ana mimba. Lakini haikuleta tofauti yoyote kwake. Yeye aliisha kuwa katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu. Hakujali dhihaka ya watu, au kicheko cha watu, wala kile walichosema juu yake. Yeye aling'ang'ania. Huyoo akakwea maeneo yenye vilima!

69 Na wanawake siku hizo hawakuwa kama walivyo siku hizi, wanatoka huku nje wamevaa kaptura; na ni siku chache kabla ya kujifungua, huko nje mtaani mbele za wanaume. Hiyo ni aibu kwa binadamu. Hiyo ni kweli.

70 Alijificha. Naye maskini Mariamu akaja kabla hajajifungua, akapanda vilima vya Uyahudi akamwone Elisabeti. Na wakati Elisabeti alikuwa amejificha, hapana shaka, asubuhi moja, akichungulia kupitia kwenye pazia, alimwona msichana huyu akija, mbio, na akatambua kwamba ni binamu ya—yake, Mariamu. Na kama vile wanawake wakati huo, walipenda kuonana, walipendana sana, alitoka mbio, labda, akamtupia mikono yake na akamkumbatia, naye alikuwa akimsalimia.

Basi akasema, "Ninasikia ya kwamba una mimba."

"Ndiyo."

Akasema, "Unajua, nina mimba, pia."

"Loo, wewe na Yusufu mmefunga ndoa tayari?"

"La, hatujafunga ndoa."

71 Na akaona alionekana ana mimba. Akasema, "Unamaanisha, mpenzi, ya kwamba wewe na Yusufu hamjafunga ndoa bado, nawe una mimba?"

"Naam."

“Litakuwaje jambo hili?”

72 “Roho Mtakatifu atatia uvuli, ataninii. . .amenitia uvuli. Sauti ya Mungu ilisema hivyo.” Kisha kasema, kasema, “Ninajua ya kwamba una mimba, pia.”

73 Akasema, “Naam, bali tayari nina miezi sita, na ni—nina wasiwasi kwa sababu mtoto hajasogea bado.”

74 Sasa, mtu yeyote anajua ya kwamba hilo si jambo la kawaida kabisa; miezi miwili ama mitatu, na uhai unahisiwa. Lakini hii ilikuwa ni miezi sita, bila ishara yoyote ya uhai. Sasa mtoto huyo mchanga alikuwa amekufa, miezi sita bila uhai hata kidogo. Akasema alikuwa ana wasiwasi juu ya jambo hilo.

75 Akasema, “Lakini Roho Mtakatifu amekuja juu yangu,” Mariamu akamwambia Elisabeti, “Roho Mtakatifu amekuja juu yangu, na amenitia uvuli; na kusema ya kwamba nitamzaa mwana, naye atakuwa ni Mwana wa Mungu, na nitamwita Jina Lake ‘Yesu.’”

76 Na mara hilo Jina la kibinadamu la Mungu, “Yesu,” lilipotamkwa kwa mdomo wa mwanadamu, kutoka kwa mwanadamu, mtoto aliyekufa akafufuka katika tumbo la uzazi la mwanamke, na akampokea Roho Mtakatifu. Na kama hilo litafanya hivyo kwa mtoto mchanga, aliyekufa tumboni mwa mama yake, linapaswa kufanya nini kwa Kanisa lililozaliwa mara ya pili? Mara ya kwanza ambapo Jina la Yesu Kristo lilipotamkwa kwa mdomo wa mwanadamu, mtoto mchanga aliyefia kwenye tumbo la uzazi la mama yake alifufuka na kumpokea Roho Mtakatifu. “Limenitokeaje hata mama wa Bwana wangu anijie mimi?” akasema Elisabeti. “Maana mara tu sauti ya salamu zako ilipoingia maskioni mwangu, kitoto changu kichanga kiliruka ndani ya tumbo langu kwa shangwe.”

77 Na leo hii tunadai kuwa na Roho huyo Mtakatifu, na tunashikwa na woga tukiwa Naye, tunaogopa kupiga hatua. Inatupasa kung’ang’ania. Kama tunaye Roho Mtakatifu aliye halisi kweli, tutang’ang’ania.

78 Sasa ninaenda mbali sana, ninaondoka, ninaliacha somo langu. Na hapa umekaribia wakati wa kuanza mstari wa maombi sasa, wala hata sijalifikia somo langu bado. Huu ni mfupi sana.

79 Mwanamke huyu tunayenena habari zake, mwanamke huyu Msirofoinike, yeye alikuwa ni Myunani, naye alikuwa amesikia habari za Yesu. Sasa, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Naye alikuwa amesikia.

80 Na, kwa namna fulani, imani huona chanzo ambacho wengine hawakioni. Huenda da—daktari akasema, “Mwanangu, nimefanya yote niwezayo kufanya kwa ajili yako.” Yeye amefikia mwisho wake. Hayo tu ndiyo mtu huyo anayoweza kufanya. Anaona kitu hicho kimeenda mbali wala hakuna kitu anachoweza kufanya kukihusu. Lakini, mnaona, imani hupata

chanzo ambacho hajui lolote kukihusu. Sayansi haitaithibitisha, kwa maana imani . . .

81 Silaha zote za Mungu ni mambo ya kimbinguni. Silaha za Mungu ni nini? Upendo, upendo ni nini? Hebu nithibitishie kisayansi kwamba kuna kitu kama upendo. Uko wapi? Ninyi, ni wangapi wanaopenda, inua mkono wako; unampenda mke wako, unampenda ndugu yako, unawapenda marafiki zako? Vema, ninataka mtu fulani, sayansi fulani, inithibitishie ni sehemu gani ya wewe ambayo ni upendo. Unaununua wapi, ni duka gani la dawa? Ninataka fungu lake, upendo. Furaha, je! una furaha? Amani, uvumilivu, upole, subira, ni kitu gani? Yote ni mambo ya kimbinguni.

82 Mungu ni wa mbinguni. Humthibitishi Mungu kisayansi. Unamwamini Mungu. Unaliamini. Usipoliamini, basi, mtu anayesema "kila kitu ambacho si cha kisayansi, si cha halisi, si kweli," basi mtu huyo hawezi kuwa Mkristo. Inambidi kuamini. Kwa imani tunamwamini Mungu; sio kwa elimu, sio kwa theolojia. "Bali kwa imani unaokolewa."

83 Angalieni, imani huona chanzo ambacho wengine hawakioni. Neno Lake ni upanga, Waebrania 4:12 ilisema hivyo, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hata huyatambua mawazo, makusudi yake yaliyoko moyoni." Hilo ni Neno la Mungu. Na kitu pekee kinachoweza kuushika huo upanga ni mkono wa imani.

84 Hakuna kitu kingine kinachoweza kufanya jambo hilo, hakuna kitu kingine. Huna budi kuona kitu fulani vinginevyo, kisayansi. Wewe, kisayansi, kielimu, huwezi kuushika upanga huo. Huwezi kufanya hivyo kwa elimu; imevurugika sana, ina utata mwingi; unalifanya, ingelifanya, itajaribu kujikana Yenyewe na kila kitu. Huwezi kufanya jambo hilo. Yesu alisema, "Limefichwa kwenu," kwa hiyo sahau hilo. Huwezi kulijua. Limefichwa. Na wakati Mungu anapoficha chochote, kimefichwa kwelikweli.

85 Hiyo ndiyo sababu umefichwa sana, kama wewe ni Mkristo. "Kwa kuwa umekufa, na maisha yako yamefichwa katika Mungu, kupitia Yesu Kristo, na kutiwa Muhuri na Roho Mtakatifu." Ibilisi atakupataje? Hawezi kukupata. Umefichwa. Mungu hukuficha. Amina. Ni mahali pa kujificha jinsi gani, kifuani mwa Yesu Kristo!

86 Sasa, imani huushika, inautumia. Sasa huenda usiwe na nguvu za kutosha, mkono huo wa imani, kukata shimo upitie humo, na kuingia ndani yake kama wengine wanavyoweza kufanya. Lakini endelea tu kugonga, itakuja. Ushikilie tu.

87 Alikuwa na vizuizi vingi, maskini mwanamke huyu Myunani, lakini imani yake haikuwa na kizuizi chochote. Imani haina kizuizi hata kidogo. Hakuna kitu kinachoweza kuizuia imani. Haijalishi mtu mwingine yeyote anasema nini, hakuna

kitu kinachoizuia imani. Hebu tuone baadhi ya "huenda ikawa" ambazo zingeweza kumpata. Huenda yeye angeninii . . .

88 Mtu fulani, huenda angemwambia, "Wewe ni Myunani. Dhehebu lako haliudhamini mkutano Wake." Lakini yeye aling'ang'ania, kwa vyovyote vile. Alikuwa anaenda, kwa vyovyote vile, maana alikuwa amesikia. "Na imani chanzo chake ni kusikia." Si kwa ushirikiano, bali kwa kusikia.

89 Angalieni, huenda walisema hivi, ya kwamba, "Wewe ni Myunani. Wewe si wa tabaka la watu wao. Wewe, kuna—kuna . . . Wana ngozi tofauti na yako. Wao ni wa jamii nyingine." Hata hivyo, hilo halikumsumbua. Hilo halikumsumbua.

90 Na baadhi yao huenda walikuja na kusema, "Sasa huo ni upuuzi. Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji huo unaosikia habari zake. Yeye ni mlokole mwingine tu ambaye ameinuka." Hakika, wana kila namna ya dola bandia, bali kuna iliyo halisi, mahali fulani, hiyo iliyoigizwa. Hiyo ni kweli. Sasa mtu amesema, "Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho. Hilo ni kundi la ulokole mtupu tu huko chini, kundi dogo tu la hao ambalo . . . Tumekuwa nao sikuzote."

91 Lakini, bado, kitu fulani kilikuwa kimemgusa mwanamke huyo; angali alikuwa aking'ang'ania. Siku za miujiza huenda zilikuwa zimekwisha kwa huyo aliyekuwa akisema naye; bali si kwake. Huenda zimepita kwa baadhi ya wenzako, bali si kwako, kama una imani.

92 Huenda kulikuwa na kundi lingine, pengine baadhi ya wanawake walisimama pembeni, wakisema, "Martha." Natumaini hakuna Martha hapa. "Martha, unajua nini? Mume wako atakuacha, kwa hakika mara utakaposhuka kwenda kwenye mkutano huo. Sasa, ninajua binti yako ana kifafa, lakini nakwambia, itakuwa . . . Kama mume wako kamwe akikugundua unashuka kwenda kule! Yeye ni mwanachama wa vilabu vikubwa na mashirika ya jijini; kama ukishuka kwenda kule, yeye atakuacha." Hilo halikumaanisha kitu kwake. Alikuwa anaenda, kwa vyovyote vile. Imani ilikuwa tayari imetia nanga. Imani haijui kizuizi chochote.

93 Vema, basi, huenda kulikuwako na kundi lingine huko chini pembeni, lililosema, "Unajua nini? Utakuwa ndiwe kichekesho kanisani, kwa maana unashuka kwenda kule bure. Na watu watajua ya kwamba unaenda. Na mara utakapojitambulisha pamoja nao, basi utakuwa ndiwe kicheko cha watu. Kila mtu atakucheka." Hilo halikumaanisha kitu kwake, hata kidogo. Alikuwa ameng'ang'ania.

94 Kundi fulani huenda lilisema, "Watakutenga kanisani mwako; watakupa kadi yako ya ushirika." Bado, aling'ang'ania. Hilo halikumzuia hata kidogo. Kwa nini? Alikuwa tayari ameikamata imani.

95 Laiti ningalikuwa na wakati wa kusimama hapa kwa saa nne na kuwaambia tu juu ya—ya matukio ya kitu kama hicho, ambapo wanawake na wanaume na watoto, waliokuwa wakifa; na, kwa taarifa za madaktari, wanaishi, usiku wa leo, kwa neema ya Mungu. Kwa sababu, kitu fulani kiliwashika, imani! Wazo ndilo hilo. Vema.

96 Yeye alikuwa amevunja na kupita malango haya yote, wakosoaji wote, vichekesho vyote, kila "mumeo atakufukuza; kadi yako ya ushirika imeondolewa kanisani, itakubidi kutafuta kitu kingine; utakuwa mtu aliyetengwa; utaitwa mtakatifu anayejifingirisha." Hilo halikumaanisha kitu kwake, kwa sababu tayari alikuwa amemwona Mungu. Alikuwa amesikia, na imani chanzo chake ni kusikia. Naye alijua ya kwamba wengine walikuwa wameponywa, kwa nini binti yake asiweze kuponywa? Haya basi, anapita.

97 Hatimaye anawasili miguuni pa Yesu, na hebu angalieni ulikuwa ni mshangao wa jinsi gani! Watu wengi hufikiri ati kwa sababu tu unaweza kufika pale, hakuna lingine la zaidi; bali ni kwamba tu umeanza sasa. Wakati alipofika kwa Yesu, ni sikitiko la jinsi gani kwake; ama lingelikuwa, labda, kwetu siku hizi. Yesu alisema hata hakutumwa kwa jamii yake.

98 Kama huyo alikuwa ni baadhi yenu Wapentekoste wa siku hizi, mbona, ungelielekeza pua yako juu hewani na kuondoka, na kusema, "Hivi hivyo ndivyo ilivyo? Kama hawanitaki kwenye Assemblies, nitajiunga na Umoja. Kama hawanipendi huko, nitaenda kwa church of God. Si lazima ni—nivumilie upuuzi kama huo." A-ha, hiyo ndiyo sababu miujiza imeondoka kanisani. Hiyo ndiyo sababu imani imehama kanisani. Mnaona?

99 Hata Yesu, Mungu Mwenyewe! Lisikilizeni. Mungu yeye yule aliyekuwa akienda kumwabudu, na—na akabadilisha mawazo yake, na akaja ku—kumwamini; wakati alipofika Kwake, alikaribishwa shingo upande.

100 Mnakumbuka nikizungumza jana usiku juu ya maua ya kuzalishwa na kadhalika? Ukristo siku hizi ni wa kuzalishwa. Si ule wa asili. Kama ulikuwa na ubatizo asilia kama waliokuwa nao kule nyuma, kanisa hilo la kipentekoste lingekuwa ninii . . . hakuna kitu kingaliweza kuuzuia. Ingekuwa ni kama nyumba inayoungua moto wakati wa kiangazi, huku upepo wenye joto ukivuma. Hakuna kitu kingeliweza kuukomesha; inawaka moto! Lakini siku hizi ni kitu gani? La, ni kundi tofauti siku hizi. Maoni yangu: ni la kuzalishwa.

Angalieni, Yeye alimkaribisha shingo upande.

101 Siku hizi inatubidi kuwabembeleza, "Nitakuahidi; kama utakuja tu huku, nitaiweka kadi yako kwenye kitabu changu hapa, barua yako, nami ni—ni—nitaona kile ninachoweza kufanya. Tutakutana na halmashauri ya mashemasi, tuone kama hatuwezi kukuingiza kwenye halmashauri ya mashemasi ama—

ama kitu fulani.” Hivyo ndivyo inavyowabidi kuwafanyia siku hizi. Mnaona ni kundi la namna gani tulilo nalo?

102 Lakini hata wakati alipofika pale, Yeye alisema, “Hata sijatumwa kwa jamii yako. Na, mbali na hayo, hao si kitu ila kundi la mbwa.”

103 Loo, jamani, sisi tungelifanya nini? Wewe ungelifanya nini? Jiulize mwenyewe hilo, na uwe mwaminifu. Mtu fulani alimdharau, mbona, kama hata huombewi, usiku wa kwanza, unadai hutarudi tena. Ndipo ati una imani? Hakika. Naam. Sasa, kumbukeni, kanda hii inaenda ulimwenguni kote. Sielekezi tu kidole changu hapa; ninakielekeza kila mahali. Mnaona? Naam, wewe, wewe hutarudi. La. Hata huwezi kuketi na kusikiliza mpaka mkutano uishe. Unaona? “Naam, nina imani”? Naam.

104 Lakini yeye aliitwa mbwa. Hicho ndicho kilicho duni kabisa kinachoweza kupatikana, ama alikuwa hivyo kwao siku hizo, mnyama mchafu. Naam, leo yeye ni kijimungu; lakini hapo mwanamke atamchukua maskini mbwa mdogo na kumpa malezi ya mama, na kupanga uzazi, maana anataka kwenda kwenye madansi na karamu, na kufanya upuuzi kama huo, naye hana wakati kwa ajili ya mtoto wake. Anajua unaweza kumweka mbwa kwenye kizimba mahali fulani, aende naye. Hiyo ni kweli kabisa, unaona. Anapanga uzazi, kisha anaenda kanisani na kuimba kwenye kwaya; anavaa kaptura, suruali, chochote kile, na kujiita Mkristo; anakata nywele zake na angali anasema ana ushirika na Mungu, wakati Biblia ilisema hana. Hiyo ni kweli kabisa. Sijali . . . Sikilizeni.

Mnasema, “Hilo jambo dogo, kwa nini unasema hilo?”

105 Hapo mwanzo, neno moja lilisababisha magonjwa yote na mauti. Mungu yeye yule, mwishoni mwa Kitabu, alisema, “Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, au kuongeza neno moja Kwake.” Kwa hiyo haidhuru unafanya nini, jinsi gani unavyodai kuwa mtakatifu, ni jinsi gani unavyoruka juu chini na kulia, kunena kwa lugha, kukimbia sakafuni, ama lolote unalotaka kufanya, ama kuwapa maskini, ama chochote ulicho; hilo silo. Umelivunja Neno hilo; na, Neno hilo moja likivunjwa, huwezi kurudi ndani! Kweli kabisa, si hata Neno moja. Unachukua kanuni za imani badala ya Neno, kwa maana inakufaa zaidi.

106 Hiyo ndiyo sababu watu wanaweza kujiunga na kanisa, na kwenda kwenye *hili*, *lile*, ama *lingine*, na kuketi kule, si kitu ila ni nyumba ya kukutania wanachama. Si kanisa. Unazaliwa Kanisani; unajiunga na nyumba ya kukutania wanachama. Lakini unazaliwa Kanisani, Kanisa, sio kanisa fulani; lile Kanisa. Kuna Kanisa moja tu. Na wewe . . .

107 Nimekuwa katika familia ya Branham kwa miaka hamsini na mitano, wala kamwe hawakuniomba nijiunge na familia hiyo. Nilizaliwa humo. Hiyo ni kweli.

Naam, akakataliwa, akaitwa “mbwa,” bali hata hivyo alishikilia.

108 Mnaona, yeye alikuwa na imani. Alivunjwa matarajio na marafiki wake wote, akavunjwa moyo na watu wake, kila aina ya mambo yakijaribu kumzuia. Lakini kila kitu kimetupwa huko. Hiyo inaonyesha Shetani akijaribu ku—kuisukumia mbali imani halisi, bali hawezi kufanya hivyo. Sijali mtu yeyote anasema nini; ingali pale. Yeye anang’ang’ania. Anaendelea kusonga mbele.

109 Akafika kwa Yesu, ndipo Yesu akasema, “Sikutumwa kwa jamii yenu. Sikutumwa kwa kanisa lenu. Wao hawashirikiani. Ninyi si kitu ila kundi la mbwa, kwa vyovyote vile.” Angali alisonga mbele! Anasema, “Mimi, nilikuja ku—kuwaponya hawa, walio Wangu; sio kuja kuwaponya ninyi. Si vizuri kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwapa ninyi kundi la mbwa.”

Akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana.” Amina.

110 Imani daima itakubali Neno ni kweli. Amina. Sasa, kama unataka kushikilia kanuni za imani, endelea; lakini imani, imani halisi ya kweli, hukubali Neno ndilo ile Kweli.

111 Akasema, “Kweli, Bwana, lakini mbwa wanaweza kula makombo yaliyo chini ya meza ya watoto.” Hilo liligonga sawa. Hilo liligonga sawa. Yeye hakuwa m—mmea wa kuoteshwa kibandani. Hakuwa ku—kundi la kuchanganywa mbegu, linalojiita waaminio, tulilo na kundi lao leo. Yeye alikuwa na imani halisi. Alikubali Yeye alisema kweli. Lakini hakuwa hata akitafuta mkate mzima ambao watoto wangekula; alikuwa tu akitafuta makombo.

112 Sisi ama tupate kilicho bora kuliko vyote la sivyo tusichukue chochote. Tutaachana nacho, na kisha tuseme, “Tuna imani. Wasiponifanyia mema, nitaondoka.” Hiyo si imani. Hiyo si imani.

113 Imani ipo. Ninachojaribu kuwaambia, enyi marafiki, tutafanya mstari wa maombi hapa moja ya siku hizi usiku. Nami sitaki kuona machela hata moja, kiti cha magurudumu kimoja, gongo moja, wala chochote kile ila viwe vimeachwa hapa sakafuni, nao wakitembea na kwenda. Mnaona? Isipokuwa uje kwa aina ya mtazamo sahihi, hutapata chochote. Hiyo ni kweli, unapita moja kwa moja na mtu fulani anakuwekea mkono, na kuendelea. Hilo, hilo si jambo zuri. Unapaswa kujua ni kwa nini umekuja . . . “Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini.”

114 Angalieni, kumbukeni, kamwe hakuwa ameona muujiza. Yeye alikuwa ni Myunani. Anajua . . . Alikuwa ni Mmataifa. Hakuwa ameuona muujiza, hata hivyo alikuwa na imani ya kwamba kulikuwako na kitu kama hicho. Na mwaka baada ya mwaka, na siku baada ya siku, tunaona miujiza, na hatuwezi kabisa kuvumilia kwa saa moja ama mbili.

115 Yeye alikuwa kama yule kahaba Rahabu. Rahabu hakutaka. . . Huyo mwanamke Mmataifa, hakutaka kuona jinsi Yoshua alivyovalia nguo zake, wala kumwona Yoshua. Alisema, “Nimesikia na ninaamini.” Hivyo tu. Yeye alisikia na alikuwa ameamini.

116 Yesu akasema, “Kwa sababu ya neno hili!” Alikuwa na mtazamo sahihi kwa karama ya Mungu. Kumbukeni, yeye alikuwa ndiye Mmataifa wa kwanza ambaye alifanyiwa mwujiza, kwa sababu ya imani yake. Imani hukubali kwamba Neno ni kweli, hujinyenyekeza, kama vile inavyofanya siku hizi.

117 Martha katika Uwepo wa Mungu. Martha, dadake Lazaro, alijinyenyekeza kwenye Uwepo wa Yesu. Naye alikuwa mng’ang’anizi wakati alipofika pale. Yeye alisema. . . Alisema, “Bwana, kama ungalikuwako hapa, ndungu yangu hangalikufa; lakini hata sasa, yoyote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

118 Yeye akasema, “Mimi Ndimi ufufuo, na Uzima; yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, ataishi; kila aishie na kuniamini hatakufa kabisa. Je! unayasadiki haya?”

119 Kumbukeni, yeye alikuwa na haki ya kumkemea. Alikuwa ameagiza aitwe, mara mbili, wakati kaka yake alipokuwa mgonjwa; akamwacha afe. Lakini, mnaona, yeye alikuwa na imani. Alijua.

120 Na kama yule mwanamke Mshunami, katika wakati wake, wakati mtoto wake alipokufa, kwamba aliamini Mungu alikuwa ndani ya huyo nabii, Eliya, naye akamshikilia Eliya moja kwa moja. Akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, na roho yako iishivyo wala haifi, sitakuacha.” Alikuwa mng’ang’anizi. Naye Eliya hakujua la kufanya. Aliingia tu mle chumbani, akatembea huku na huku, mpaka Roho wa Mungu, Uwepo wa Mungu, ukashuka. Akajilaza juu ya mtoto huyo mchanga, akapiga chafya mara saba akafufuka. Kwa sababu, mtu fulani alikuwa aking’ang’ania, mtu fulani alikuwa ameshika imani, apate kumfikia mtu wa Mungu.

121 Naye alijua, kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya, ni zaidi sana jinsi gani alivyokuwa katika Mwanawe Mwenyewe. Alijua. Imani chanzo chake ni kusikia. Na katika Uwepo wa Yesu, alikuwa mng’ang’anizi.

122 Yesu, ilionekana, alijaribu kumfukuza, na kusema, “Yeye atafufuka,” na yote *haya*, na kadhalika. Lakini alikuwa mng’ang’anizi. Alisukuma kupitia kila mkosoaji akisema, “Sasa uko wapi ule mfumo wa uponyaji wa Kiungu uliokuwa ukizungumzia? Uko wapi huo wote? Ndugu yako amekufa na kuzikwa huko nje sasa. Naye Mchungaji aliondoka kisiri mjini mpaka huyu akafa, na kisha akarudi.” Lakini hilo halikumzuia. Alisukuma moja kwa moja akipita kila mkosoaji mpaka akamfikia Yeye. Akapata kile alichoomba.

123 Sasa hapa wakati fulani uliopita, ndio kwanza nikumbuke, maskanini. . .Ninaona baadhi ya hao ndugu wameketi hapa kutoka maskanini, usiku wa leo. Kulikuwako na mama mmoja. . .Nilikuwa nimekuja kanisani. Nasi tuna, karibu kila usiku, tuna karibu kadiri ya wale tulio nao hapa ndani mkutanoni mwetu. Na kwa hiyo basi tulikuwa. . .Si—sikuwa nikiwaombea wagonjwa usiku huo. Na kulikuwako na mwanamke aliyetoka California, aliyekuwa na uvimbe, uvimbe wenyewe ulikuwa na uzito wa ratili hamsini. Na kwa hiyo walikuwa wamemweka huko nyuma. Na kwa hiyo wakamwambia hatukuwa tuwaombee wagonjwa usiku huo; ilikuwa ni kushuka tu kuja kuhubiri, maana ilikuwa ndio tu nimetoka mkutanoni.

124 Ndipo nilipotoka kwenye mlango wa nyuma, mashemasi wawili walikuwa wamemzungusha nyuma ya nyumba, kwenye kiti, na kumketisha mlangoni, na moja kwa moja sakafuni. Basi nilipotoka, alinishika kwenye mguu wa suruali nilipotoka. Akasema, "Ndugu Branham, jambo pekee ninalokuomba, ni uniwekee mikono yako." Akasema, "Uvimbe wangu utaondoka." Naye alikuwa karibu tu *hivi*.

125 Kama majuma sita kutoka wakati huo, alikuwa kwenye mkutano, nasi tukawachukua kina dada waende wakamchunguze. Pasipo na kufanyiwa upasuaji wowote, hapakuwapo na kivimbe chochote mahali popote. Haidhuru kama haukuwa ni usiku wa kuwaombea wagonjwa, yeye alikuwa mng'ang'anizi. Alipata kile alichoomba. Imani ilikuwa imepata mahali pake, na ikashikilia.

126 Mikaya. Nami ninafunga katika dakika moja. Mikaya, mbele ya makuhani mia nne waliofunzwa vizuri, manabii wa Kiebrania pamoja na yote. Yeye alisema, "Shuka uje huku, Mikaya, umetengwa na shirika la wahudumu hapa chini; lakini kama utasema jambo lile lile wanalosema sasa, na useme Ahabu akwee, pamoja na . . . Ahabu na Yehoshafati wakwee; nasi tunatambua ya kwamba, ya kwamba watakurudisha kwenye ushirika."

127 Akasema, "Kama Mungu aishivyo, mimi nitasema tu yale aniambiayo." Mungu, tupe Mikaya wengine zaidi! Mnaona?

128 Kwa hiyo, akangoja. Usiku huo ono likaja. Akalichunguza ono lake na Neno. Maana, Neno la Mungu lilikuwa limesema ya kwamba, Ahabu, ya kwamba mbwa watairamba damu yake, kama vile walivyoiramba ya Nabothi. Kwa hiyo tunaona ya kwamba ono lake lilikuwa limelingana kabisa na Neno.

129 Kwa hiyo yeye alikuwa mng'ang'anizi wakati alipotoka nje kesho yake asubuhi. Kasema, "Kwea, lakini niliwaona Waisraeli wametawanyika mlimani, bila mchungaji."

130 Naye huyu kuhani mkuu, ama kiongozi wa manabii, akaenda pale, akampiga kofi la mdomoni, na kusema, "Roho wa Mungu

alienda wapi wakati alipoondoka kwangu?” Bado Mikaya hakujali yale waliyosema. Alisimama pale. Akasema, “Mweke jamaa huyu kortini,” kasema Ahabu, “na mwekeni kwenye korti ya ndani, na mumlishe mkate na maji ya shida. Atanijuta wakati yeye . . . wakati nitakaporudi,” kwa maneno mengine, nitamkata kichwa, ama kitu kama hicho.

131 Akasema, “Kamwe ukirudi, Bwana hajasema nami.” Loo, alijua mahali alipokuwa amesimama. Haileti tofauti yoyote yale hao wengine waliyowazia; yeye alijua aliishakuwa katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa ameisikia sauti ya Mungu. Ilikuwa sawasawa kabisa na Neno la Mungu.

132 Ndivyo itupasavyo sisi, usiku wa leo, kuiona saa hii tunayoishi, na kuiona ahadi ya siku hii, ambayo Neno la Mungu liliahidi. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini; Neno lilisema hivyo, na Yesu anakuja kujitambulisha. Anayeng’ang’ania!

133 Yule kipofu ambaye Yesu alificha . . . au alimponya; asingeweza, asingeweza kuelezea ama kubishania theolojia yao. Lakini jambo moja alilojua, yeye alikuwa mng’ang’anizi.

134 Baba yake na mama yake wasingeweza kusema. Walisema, “Vema, tunaogopa watatutenga na sinagogi.” Nao wakasema, “Mwulizeni, yeye ni mtu mzima.”

Akasema, “Ati ni nani aliyekuponya?”

Akasema, “Mtu yule, Yesu wa Nazareti.”

135 Akasema, “Mpe Mungu sifa!” Kasema, “Tunajua mtu huyu ni mwenye dhambi.”

136 Akasema, “Sasa, kama Yeye ni mwenye dhambi, ama sivyo, mimi sijui. Siwezi kusema hilo. Lakini,” kasema, “jambo moja ninalojua, wakati mmoja nilikuwa ni kipofu, sasa ninaona.”

Wao wakasema, “Hatujui anakotoka Mtu huyu.”

137 Anasema, “Hii ni ajabu. Mnapaswa kuwa ndio viongozi wa siku hizi, mkijua mambo yote ya kiroho; na hapa Mtu mmoja anakuja na kuyafumbua macho yangu, ambapo nilizaliwa kipofu, na hata hivyo ninyi hamjui atokako?” Loo, alikuwa mng’ang’anizi, hakuna kitu kitakachomsumbua. Alikuwa akizungumza na Mungu.

138 Nathanaeli hakujali, kumwita, “Bwana, Mfalme wa Israeli,” mbele ya mchungaji wake na hao wengine wote, wakati alipomwambia mahali alipokuwa si—siku moja kabla. Nathan hakujali.

139 Yule mwanamke kisimani hakujali ni watu wangapi waliomwambia haikuwa ni halali kwake kusema chochote sababu alikuwa ni kahaba. Alikuwa amekutana na Mtu ambaye alikuwa akimtazamia, tangu alipokuwa m—msichana mdogo, akijua ya kwamba Yesu alikuwa aje jukwaani, Nabii. Naye

alikuwa amempata huyo Nabii ambaye alimwona akimwambia mambo aliyokuwa amefanya. Ati umnyamazishe? Kama ninavyosema tena, kama nyumba inayoungua katika upepo mkali. Usingeweza kumnyamazisha. Moyo wake ulikuwa ukiwaka kwa shangwe na amani. Alikuwa amesamehewa dhambi zake. Alikuwa amemwona Masihi. Alikuwa ameuona Uwepo Wake. Alikuwa ameliona Neno Lake.

140 "Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe? Huna budi kuwa ni nabii Wake."

Akasema, "Mimi Ndiye."

141 Na kama Mtu huyo aliweza kufanya jambo kama hilo, asingedanganya, alijua huyo alikuwa ni Masihi, kwa hiyo habari njema ilibidi kutangazwa.

142 Jinsi gani tunavyopaswa kuwa na moto ule ule usiku wa leo, tuking'ang'ania kumfanya kila mtu ajue ya kwamba Roho Mtakatifu ni halisi leo, ya kwamba Yeye anatushukia na kufanya jambo lile lile alilofanya, na ahadi za wakati huu. Sisi hatung'ang'anii. Sijui kama kweli limetuingia kabisa? Unaona, mwangalie yule mwanamke pale kisimani.

143 Jambo moja, sina budi kufunga. Nina kama nusu ukurasa wa mihtasari pale, bali ninataka kufunga kwa kusema jambo hili. Hili linaniletea hadithi fulani. Ndipo tutawaombea wagonjwa. Tutachelewa kidogo tu, lakini labda dakika kumi, kumi na tano, bali nivumilieni muda kidogo tu zaidi.

144 Nilikuwa huko kwenye Jiji la Meksiko kama miaka mitatu iliyopita. Ni wangapi wanaomjua Ndugu Espinoza, ninyi Wahispaniola hapa? Vema, nadhani ni wengi wenu. Yeye alikuwa mkalimani wangu. Tulikuwa huko chini kwenye Jiji la Meksiko. Nilikuwa, kadiri wajuavyo, Mprotestanti pekee aliyepata kufika kule, akidhaminiwa na serikali. Lakini Jemadari Valdivia, mnamkumbuka, ni mmoja wa Wafanya Biashara Wakristo, alikuwa amepokea, alikuwa ameokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu, naye alikuwa amepitia serikalini na kuniingiza kule.

145 Na kwa hiyo tukapata uwanja mwingine mkubwa mduara kule. Ulienea watu elfu kadhaa; haukukaliwa na mtu, ilibidi watu wasimame. Na ninyi—ninyi mnawazia kuhusu kusimama hapa kwa saa mbili ama tatu kwenye chumba hiki, hao watu walisimama kwenye hilo jua kali lichomalo la jangwani, pale kutoka saa tatu asubuhi, hadi saa tatu usiku huo, siku baada ya siku. Ndipo, usiku mmoja, mvua ikinyesha kwa fujo, wao walisimama pale; na hao wanawake vijana wa Kimeksiko, nywele zao zikining'inia usoni mwao, nayo ikinyesha kwa nguvu sana nisingeweza kuona nusu ya wasikilizaji. Haikuleta tofauti yoyote kwao; walikuwa wamelishikilia Neno hilo la Uzima.

146 Ninakumbuka usiku mmoja pale, nikiingia. Nilikuwa tu kule siku tatu usiku. Jukwaa refu kama hili, ama labda ni refu zaidi

kidogo. Kulikuwako na mzee mmoja kipofu aliyekuja jukwaani, nao walikuwa wamemleta humo.

147 Jamaa aliyekuja na kunichukua, nilimwita *Mañana*, hilo linamaanisha "kesho." Alikuwa mambo yake ni ya polepole sana! Kamwe asingeweza kufika pale, na, vema, angeangalia huku na huko, na kufika pale wakati wowote. Nami nikiomba, naye . . . Ndipo nilimwita tu "Mañana"

148 Kwa hiyo walikuwa wamenipandisha nyuma ya ukuta huu mkubwa, kwa ngazi, na kisha kunishusha jukwaani. Ndugu Jack Moore, ni wangapi wanaomjua? Hakika, nadhani mnamjua, na Ndugu John Sharrit na wengi wao hapa. Walikuwa pale jukwaani. Usiku huo, akija jukwaani . . .

149 Mañana alisambaza tikiti, ka—kadi za maombi, lakini Billy alitembea moja kwa moja karibu naye kuhakikisha ya kwamba kila kitu kiliendelea vema. Yeye angeweza kuzungumza nao na kuwapa kadi za maombi, bali Billy alienda kuona kama ilikuwa ni sawa kweli ama si sawa, kama angeuza yoyote ya hizo, ama kile angefanya, ama kumpendelea mtu; kuacha kila aliyetaka kadi ya maombi aipate.

150 Kwa hiyo usiku huo wakati kadi za maombi zilipoitwa, kulikuwako na mzee mmoja aliyekuja jukwaani, miguu mitupu, na miguu ya suruali yake yote imeraruka, kofia chakavu mkononi mwake, imefungwa kwa kamba. Ndipo aliponikaribia, yeye alikuwa ni kipofu, nami nikamwangalia maskini mzee huyo. Nami nilikuwa nimesimama pale, nguo nzuri kama nilizo nazo usiku wa leo, mtu fulani alikuwa amenipa suti nzuri mpya, nilikuwa nimevaa viatu vizuri. Na maskini mzee huyo pale, shati chakavu, na amejaa mavumbi. Huyo hapo, kipofu kabisa, macho yake karibu yote ni meupe kama shati langu kwa watoto wa macho. Ndipo, na nikawazia, "Ni jambo katili jinsi gani Shetani amefanya!" Maskini mzee huyo labda hajapata kula mlo mzuri, maishani mwake.

151 Uwiano wa uchumi ni mbaya sana kule. Nao, hebu wazieni tu sasa, tuseme, Pedro, Petro, yeye—yeye ni—yeye ni mwashi, anapata peso thelathini kwa siku, lakini inawabidi kufanya kazi siku nne ajinunulie jozi ya viatu. Mnaona? Na vipi kuhusu maskini Pancho, ama Chico, maskini huyu anayefanya kazi hapa nje na kupata tu peso nne kwa siku, akiwa na watoto wanne ama watano wa kulisha? Angeshuka aende na kununua chapati chache za haragwe la amiba kwa ajili ya watu wake, na usiku wa leo Martina anaweza kula moja na—na mtoto Chico anaweza kula moja, lakini mtu mmoja hana budi kula moja . . . kwenda bila kula. Inawabidi kuweka akiba kiasi fulani, wapate kununua mshumaa wa shahamu wakauwashe kwenye madhabahu ya dhahabu, kwa ajili ya dhambi zao. Hicho ndicho kinachoniuma moyo. Kwa hiyo haya basi.

152 Sasa, maskini jamaa huyu mzee alisimama pale, naye alikuwa akisema kitu katika Kihispaniola. Naye alikuwa na shanga nyingi zilizozungushwa kwenye vidole vyake, nami nikamwambia, "Ziondoe," na kupitia kwa Ndugu Espinoza.

153 Basi nikawaza, nikawazia, "Nitainua mabega yangu. Ninaweza tu kuvua koti langu, na kumwambia. Na mabega yake ni mapana zaidi kuliko yangu." Nikasogeza miguu yangu karibu na yake, nikawaza, "Ningeweza kuvivua viatu vyangu upesi, wala hakuna mtu angaliona hilo, na nimpe viatu vyangu," lakini miguu yake ilikuwa ni mikubwa zaidi. Basi nikawaza, "Vema, ningefanya nini?" Nikawaza, "Ee Mungu!"

154 Kama huwahurumii watu hakuna haja ya kujaribu kuwatumikia. Inakubidi kuwahurumia. Hiyo ndiyo sababu Yeye alichukuana na mambo ya udhaifu wetu.

155 Nilimkumbatia tu, namna *hii*, na nikasema, "Baba wa Mbinguni, kama baba yangu angaliishi, angekuwa na karibu umri huu. Huyu ni baba wa mtu fulani." Nami nilikuwa nimesimama tu pale namna hiyo, nami nikamsikia akipaza sauti, "Gloria a Dios!" Hiyo ni kusema "Utukufu kwa Mungu," unajua. Nikaangalia kote kule, na mzee huyo aliweza kuona vizuri kama mimi, akitembea tu huku na huku jukwaani, akiendelea tu. Vema, na, hakika, iliwabidi kuwaleta mabawabu, karibu mabawabu mia tatu ama mia nne wakisimama pale, kuwatuliza. Ndipo iliwabidi kunirudisha kwa kuninyanyua kwa kamba.

156 Kesho yake usiku, niliingia mle, kulikuwako na malundo juu *hivi*, lundo, huku na huku pale, la shali chakavu na kofia na kadhalika, walizokuwa wameweka pale ziombewe. Jinsi walivyopata kujua ipi ni ya nani, sijui mimi, zote zimelundikwa pale, zimewekwa pale. Na ilikuwa inanyesha. Nilikuwa nimechelewa. Ndipo nikaingia pale, nami nikaanza tu kuhubiri. "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana," na Ndugu Espinoza akiwa pale akifasiri.

157 Ndipo Billy akaja hapo na kunigusa begani, akasema, "Baba, itakubidi kufanya jambo fulani." Kasema, "Mañana tayari amesambaza kadi zote za maombi." Kisha kasema, "Yupo maskini mwanamke anayesimama pale, mama mdogo," kasema, "ana mtoto aliyekufa, naye alikufa asubuhi ya leo."

158 Mliona makala hayo kwenye Wafanya Biashara Wakristo. Pia, kumbukeni, hayo hayana budi kuhakikishwa rasmi kabla hayajachapishwa. Daktari hana budi kutia sahihi taarifa hii, kwamba ni kweli, unapoichapisha.

159 Basi akasema, "Yuko kule, ana mtoto mchanga aliyekufa," akasema, "alikufa asubuhi ya leo." (Na ilikuwa kama saa tatu na nusu, wakati huo.) Kasema. . . (Na yapata wakati huu wa usiku.) Kisha kasema, "Alikufa asubuhi ya leo." (Alikuwa amesimama kwenye mvua hiyo pamoja naye siku nzima, naye

hakujua Espinoza alikuwa, ama, namaanisha, Mañana alikuwa akisambaza hizo kadi za maombi.) Ndipo kasema, "Hana kadi ya maombi." Kasema, "Ninao mabawabu arobaini ama hamsini, hawawezi kumzuia asiingie jukwaani." Kasema, "Atapitia moja kwa moja chini yao, anawavuruga, anapanda migongoni mwao, ama chochote kile, huku, anajaribu kufika hapa juu."

160 Ndipo nikasema, "Vema, nitakwambia." Nikasema, "Njoo hapa, Ndugu Moore." Mnajua, ninyi nyote, wengi wenu mliinua mikono yenu, mnamjua Ndugu Jack Moore. Nikasema, "Ndugu Moore, yeye hajui mimi ni nani. Hajui. Kumekuwako na wahudumu wengi wamesimama hapa, wakihubiri, Wabaptisti wengi na kila kitu, wanaoudhamini mkutano huu." Ndipo nikasema, "Sasa, wewe, nenda kule na umwombee mtoto huyo mchanga, naye hatajua tofauti, unaona."

Akasema, "Vema, Ndugu Branham."

161 Akaanza kuondoka jukwaani, kufikia umbali kama wa ule ukuta pale, ndipo nikageuka. Watu hawakujua, maana hawakuelewa Kiingereza. Ndipo nikasema, "Sasa kama nilivyokuwa nikisema, imani ni ku-. . . " Ndipo nikaangalia hapa mbele yangu, nami nikamwona mtoto wa Kimeksiko, mwenye uso mweusi hana Meno, ameketi tu pale akiniangalia kwa tabasamu, papa hapa mbele yangu.

162 Nikasema, "Ngoja kidogo, Ndugu Moore." Nikasema, "Mwambie maskini mama huyo aje hapa."

Naye Billy akasema, "Baba, yeye hana kadi ya maombi."

Nikasema, "Nimeona ono sasa hivi tu, Billy."

163 Na kwa hiyo wakashuka wakaenda kule na kumleta maskini mama huyo. Huyu hapa akaja, akikimbia kule juu, akapiga magoti, akaanza kupiga makelele, "padre," ambalo maana yake ni "*baba*," mwajua; nikamwomba asimame, Ndugu Espinoza. Ameshika mtoto; naye alikuwa amemfunika kwa blanketi dogo la bluu, lenye milia, limelowa maji kabisa, na maji yakitiririka, nazo nywele zake zimening'inia chini. Maskini mama mdogo mrembo, labda ni mtoto wake wa kwanza, alikuwa kwenye ninii wake. . . umri wa miaka ishirini na miwili ama ishirini na mitano, ameshika kitu hicho kidogo namna hiyo; umbo dogo, urefu kama *huo* na baridi, chini ya blanketi hili. Nikawaza.

164 Wote walidhani nilikuwa tu nikiomba, nipate kumwondoa, mwajua, kumwondoa mikononi mwao pale.

165 Basi nikaweka mikono yangu juu ya mtoto huyo mchanga, na nikasema, "Baba wa Mbinguni, sijui kwamba—kwamba huyu ndiye yule mtoto; lakini niliona ono pale, dakika chache zilizopita, la mtoto mdogo wa Kimeksiko, ilionekana kama mtoto mdogo mweusi, akitabasamu." Kisha nikasema. . . Wao hawatafsiri maombi, unajua. Basi nikasema, "Nilimwona akitabasamu." Nikamwekea tu mikono yangu, namna *hii*, katika

Jina la Yesu Kristo, kuomba, ndipo mtoto huyo akatupa teke na kuanza kulia kwa nguvu alivyoweza . . . Na kwa hiyo akaanza kulia kwa sauti kuu.

166 Ndipo nikasema, "Ndugu Espinoza, usiandike hilo sasa. Mtume mpiga mbio, pamoja na mtoto huyo mchanga na mwanamke huyo, umpeleke kwa daktari huyo." Ndipo usiku huo, walimwita daktari huyo, daktari akatia sahihi taarifa ya kwamba mtoto huyo alikufa kwa nimonia, asubuhi hiyo kwenye hospitali yake, ama ofisini mwake, saa tatu; na hapa ilikuwa karibu saa nne usiku huo, alikuwa amekufa tangu asubuhi hiyo, na akafufuka; naye yu hai leo kwa utukufu wa Mungu.

167 Kwa sababu gani? Yeye aling'ang'ania tu kama maskini huyu mwanamke Msirofoinike alivyong'ang'ania hapa, tunayenena habari zake usiku wa leo. Inaonyesha ya kwamba Mungu angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jambo lilikuwa ni kwamba, (ilikuwa ni kitu gani?) alikuwa amesikia habari za yule mzee kipofu.

168 Yeye alikuwa ni Mkatoliki, kwa imani. Wote ni Wakatoliki, kwa hiyo unapozaliwa Meksiko unakuwa Mkatoliki moja kwa moja.

169 Kwa hiyo basi hao watu hapo walikuwa wamemwona mzee huyu kipofu mtaani, akitoa ushuhuda wake. Yeye, walikuwa wamesikia habari zake. Mwanamke huyu hakuwa ameona kamwe muujiza. Lakini alijua kama Mungu angeweza kuyafumbua macho ya kipofu, Yeye angeweza kumfufua mtoto wake, kwa sababu ilikuwa ni Yesu Kristo yeye yule. Wakati mwingine angewafanya Wapentekoste wajisikie duni. Na hiyo ni kweli, kwa imani kama hiyo, kwa kuwa alikuwa aking'ang'ania kwamba hapana budi ilikuwa Mungu Ndiye aliyeweza kuyafumbua macho. "Na kama ilikuwa ni Mungu angedumisha Neno Lake na kuyafumbua macho, Yeye angeweza kufufua wafu." Naye alitenda hilo kwa sababu aling'ang'ania. Ningekuwa kule usiku mmoja zaidi, naye huenda . . . Huo ulikuwa ndio usiku kwa ajili yake.

170 Hivi na sisi, usiku wa leo, marafiki, hivi hatutakuwa wang'ang'anizi. Je! hatuwezi kusonga mbele tukapita kwenye magonjwa ya kutisha yasiyofahamika na kumkubali Yesu Kristo kama—kama Mponyaji wetu? Hivi hamwezi kufanya hivyo?

Na tuombe.

171 Bwana Yesu, Ee Mungu, si—sijui niseme nini zaidi. Ninaomba, Mungu, je! niitishe mstari mdogo tu wa maombi, Baba? Na labda utawaonyesha watu ya kwamba, utafanya jambo fulani kama tu ulivyofanya kabla ya ninii Yako—mauti na kuzikwa Kwako; kwamba leo hii na wakati huu, labda kungekuwako na wageni hapa, tupate kuona ya kwamba Wewe ungali ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ukilidumisha Neno Lako. Na labda kutakuwako na mtu fulani mwenye imani ya

kutosha kuvuka kizuizi hicho huko ng'ambo, hicho kizuizi cha sauti, hicho kizuizi cha dhambi, hicho kizuizi cha kutokuamini huko ng'ambo, apenye kupitia hicho, afikie mahali ambapo yote yanawezekana. Tujalie, Bwana. Tunaambiwa ya kwamba wakati hiyo ndege inapovuka hicho kizuizi cha sauti, spidi yake na nguvu zake ni kubwa sana. Mungu, tukiweza tu kuvunja hizo nguvu za kutokuamini, miujiza na kadhalika, na ahadi za Mungu, hazina kipimo, "kwa maana mambo yote yanawezekana kwake aaminiye." Tujalie, Baba. Tunaomba hayo katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo. Amina.

172 Kama nimechelewa tu kidogo, je! ni sawa kuendelea na tuwe na, tuitishe mstari mdogo wa maombi? Ninajua watu wanahangaika, lakini hebu na tuitishe tu mstari mdogo wa maombi. Hebu tuone, Jumatatu usiku tulikuwa na za A, hiyo ilikuwa ni kweli, tulipozisambaza kadi za maombi? Ama, la, ninamaanisha Jumatano usiku. Nafikiri kuhusu Jumata-. . . Jumatano usiku ilikuwa ndio usiku wa kwanza, zilikuwa ni za A, na jana usiku zingekuwa ni za B, ndipo usiku wa leo ingekuwa ni za C. Tuliita kutoka moja hadi ishirini na tano, katika A. Nafikiri hiyo ilikuwa ni sawa, sivyo, moja hadi ishirini na tano, katika A? Hiyo ni kweli, moja hadi ishirini na tano, katika A? Moja hadi kumi na tano, katika A.

173 Vema, hebu na tuite katika za B, kadi za maombi za jana, basi. Hebu tuite B, sabini na tano mpaka mia moja. Kadi ya maombi B. Tutafikia C zenu na hizo zote. Tuko kwenye B, ishirini na tano. . .La. B, sabini na tano, ninaamini ndivyo nilivyosema, sivyo? B, sabini na tano hadi mia moja. Vema. Hebu na wasimame upande *huu* sasa. B, sabini na tano hadi mia, simameni upande huu. Njoni moja kwa moja upande huu na mpange mstari hapa, baadhi yenu ndugu shukeni chini. Billy, Roy, baadhi yenu shukeni mwende pale mhakikishe watu wanaingia katika mstari wa maombi. Vema.

174 Ninataka usikivu wenu mkamilifu kwa dakika moja. Sasa iweni na kicho sana. Sasa angalieni, baadhi ya watu wanaenda na kusema, "Mhubiri alikuwa amevaa tai mbaya. Ana suti isiyo sahihi. Namna yake si nzuri. Yeye hasimami wima vya kutosha." Vema, mnaona, ungali huna imani yoyote. Unaona?

175 Kama mtu angeliingia kwa mlango ule wa nyuma pale na kuwaambia ya kwamba alikuwa na ninii. . .ya kwamba wao, alikuwa na hawala ya fedha ama hundi ya benki kwa ajili yako, ya dola milioni moja, usingejali kama alikuwa na elimu ama hakuwa nayo, usingejali kama alikuwa na ovaroli ama alikuwa amevaa koti rasmi, usingejali kama alikuwa ni mweusi, manjano, hudhurungi, mweupe.

176 Sio mjumbe; Ujumbe ndio unaopaswa kuusikiliza. "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ni wangapi wanajua hilo? Sasa kama mtaninii tu—ninii tu . . .

177 Kama—kama fundi wa mitambo pale, nafikiri, Bw. Ruby, ama nafikiri ndilo lililokuwa jina lake, niliyekutana naye hivi majuzi usiku, kama ataninii tu . . . Yeye ametupa taa, na kadhalika, hapa, kama tu atatuvumilia dakika chache kwa ajili ya Injili.

178 Sasa kila mtu awe na kicho kabisa, bali uwe mng'ang'anizi kabisa. Kazeni mwendo moja kwa moja mvuke ng'ambo ya pazia.

179 Sasa wakati Yesu Kristo anapowaponya wagonjwa. Sasa, sisemi wataponywa; siwezi kuwaambia hilo. Kumbukeni, mimi sina nguvu za kuponya. Sina nguvu, wewe huna nguvu yoyote, hakuna mmoja wetu aliye nayo. Tuna mamlaka. Ni wangapi wanaoelewa hilo?

180 Angalieni hapa, hebu niwaulizeni jambo fulani. Hapa nje mtaani, kwenye barabara hii kuu inayotumiwa sana iliyo mbele ya barabara hii kuu mno, tulipokuwa huko nje kwenye—kwenye kile kizuizi kikuu cha kulipia ushuru barabarani, ninaona kikomo cha spidi ni maili themanini kwa saa. Kuna magari yanayoshuka kupitia pale, popote kati ya nguvu farasi mia mbili, mpaka—mpaka—mpaka nguvu farasi mia tatu au mia nne.

181 Basi namba sabini na sita, naomba uje. Wanahitaji namba sabini na sita. B, sabini na sita, huenda ikawa ni kiziwi. Angalieni kote. Loo, samahani. Vema. B, sabin- . . . Hiyo ni sawa, ndugu yangu? B, sabini na sita. Vema.

182 Sasa angalieni, kwa mfano, huyu hapa maskini polisi anakuja hapa nje kwenye barabara kuu, yeye ni mdogo sana mpaka kofia yake imelalia kwenye maskio, na hana uzito wa zaidi ya ratili mia moja. Sasa ana nguvu kiasi gani kusimamisha moja la magari hayo? Na hapo baadhi yao yamepangana matatu ama manne sambamba, yanatiririka kwenye barabara hiyo kuu mbio yawezavyo, kila moja la hayo likiwa na nguvu farasi mia tatu. Asingeweza kusimamisha hata nguvu farasi moja. Na haya hapa hayo magari. Lakini acha hiyo beji kubwa imulike, na hebu ainue mkono huo! Huenda asiwe na nguvu, bali ana mamlaka. Sikilizeni hizo breki zikialika, na kuteleza kando, na kila mtu anasimama. Kwa nini? Kwa sababu ana mamlaka.

183 Mimi sina nguvu zozote. Wewe huna nguvu zozote. Ila tuna mamlaka, amina, ile beji ya imani inaning'inia kwenye Neno, "Ninaliamini. Ni la Kweli." Hiyo ndiyo inayosimamisha. Ndipo unaweza kung'ang'ania.

184 Maskini polisi mdogo akisimama pale nje na kupiga filimbi hiyo ndogo na kuinua mkono wake, nitawaambia, kila kitu kitasimama. Ni mamlaka yake. Ni mamlaka yake, kuamini.

185 Sasa mnaamini, kila mmoja wenu. Sasa mkisimama mle ndani, sasa msife moyo, ninii tu—kaeni tu hapo na mkazane kupenya ndani, mseme, "Bwana, mtu huyu hajui kitu juu yangu.

Nina hakika ya hilo. Kama anaweza kunena, kuniambia, nita—nitaamini kwa moyo wangu wote.” Sasa tungejua nini sasa?

186 Mponyaji ni nani? Yesu Kristo. Hiyo ni kweli? Vema, basi, kama Yeye yupo hapa, vema, jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kumwomba tu. “Naye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.” Hilo ni kweli? Vema. Basi, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Leo hii Yeye ni Kuhani Mkuu. Vipi, alifanyaje wakati mwanamke alipoligusa vazi Lake miaka elfu mbili iliyopita? Aligeuka na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini, na akasema imani yake ilikuwa imemponya. Hiyo ni kweli? Vema, Yeye ni yule yule leo, ingembidi kufanya vile vile, maana Yeye ni yeye yule.

Sasa je! mstari wenu wa maombi uko tayari?

187 Sasa huyu hapa mwanamke anayekuja hapa juu. Nijuavyo mimi, si—sijapata kumwona. Hatufahamiani kabisa, nijuavyo mimi. Sisi hatufahamiani. [Huyo dada anasema, “Nilikuwa mkutanoni mwako, 1947, 1950 hadi ’53.”—Mh.] Amesema alikuwa kwenye mikutano yangu mwaka wa ’47 na ’53.” Lakini. . .[“’51 hadi ’53.”] ’51 hadi ’53. Lakini kukujua wewe, sikujui. [“La,”] La.

188 Mnaona, ni kama tu—kama ningekutana nawe juma moja ama majuma mawili tangu sasa, labda kamwe nisingeweza kukujua. Kumekuwako na watu wengi sana ambao wamekuwa mikutanoni, makumi elfu tangu wakati huo, mnaona, wala nisingejua. Lakini kuhusu kile ninachomaanisha, je! ninakujua, “unanijua mimi,” unanifahamu kwa kuwa umekuwa mkutanoni. Lakini mimi kukujua, ama kujua shida yako ni nini, ama kile umefanya tangu sasa hivi na wakati huo, ama kabla ya hapo, ama kile unachotarajia kufanya, hakika, nisingejua. La.

189 Lakini sasa kusudi tusichukue muda mwingi na kila mtu, kujaribu kuninii. . .Hivi majuzi usiku, ni—nilisimama mapema. Sikuona, si—si—sikufikiri kulikuwako na wengine zaidi waliosalia. Niliacha wawili ama watatu wamesimama mstarini, sikupaswa kufanya hivyo. Kweli sikulifanya. Sijui ni kwa nini. Ninaninii tu. . .Vema, kila mtu, ilionekana kana kwamba ilikuwa ni upeo wa wakati. Hutaki kuwabembeleza watu. Unataka wawe wajasiri vya kutosha kuunyosha mkono juu kule na kushika kile unachosema, mnaona, na ndipo wanaponywa. Kama hukufanya hivyo, mbona, wao ha—hawaponywi.

190 Sasa mama huyu hapa, wakati wetu wa kwanza kukutana. Sasa kama Yeye ni “yeye yule jana, leo na hata milele,” sasa kama alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, kupitia kwa mtu mzuri aliyenipa suti hii, sasa kama Yeye angekuwa amesimama hapa amevaa suti hii, je! angeweza kuwaponya? La. La. Yeye amefanya hivyo tayari, unaona, “Alijeruhiwa kwa

makosa yetu." Asingeweza kukuponya. Ni wangapi wanaojua hilo kwamba ni Kweli? Uponyaji umefanyika tayari.

191 Mwenye dhambi yeyote hapa, Yeye asingeweza kukuokoa; amekuokoa tayari. Huna budi kuukubali.

192 Sasa kama Yeye alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, ambayo alinipa, angeweza. . .Jambo pekee angaliweza kufanya, ingekuwa ni kusema. . .Kama ungesema, "Mimi ni mgonjwa. Nina haja. Ama, nina mpendwa aliye mgonjwa," ama chochote kile, "Nina shida ya fedha. Ni—nina shida ya kinyumbani," ama chochote kile. Asingeweza, asingeweza kukupa. Angekwambia tu ya kwamba tayari amekinunua. Sasa ni wangapi wanaofahamu hilo? Hiyo ni kweli, mnaona, mnaona, maana imefanywa tayari. Mnaona? Hawezi kufanya . . .

193 Kama umekombolewa kutoka kwenye kitu chochote, mwe—mweka rehani hawezi kukushikilia tena, kama umekombolewa. Kama unayo risiti, ya kwamba kimekombolewa, hiyo yatosha. Hawezi kukishikilia tena.

194 Tunayo Risiti, mnaona; laiti mngelikuwa na imani ya kuitumia! Mnaona? Lakini sasa kama Yeye angekuwa amesimama hapa, nami nikiwekea msingi kampeni zangu zote juu ya, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," Yeye angejua shida yako ilikuwa ni nini. Na hilo hakika lingeninii. . .Pasipo mimi kujua hilo, hakika ingetambulisha kwamba ingebidi iwe ni Yeye. Ingebidi iwe ni nguvu fulani, nguvu fulani. Inategemea unawazia hizo nguvu zingekuwa ni nini. Maana, unajua ya kwamba sikujui mimi, tukizungumza kibinadamu. Na ingebidi iwe ni nguvu fulani. Na kama unaamini huyo kuwa ni Yeye. . . Na kama hukuamini kwamba ni Yeye, hakika, hupaswi kuwa umesimama hapa. Na, lakini, kama kweli unaamini kwamba ni Yeye, basi kama angeweza kukwambia yale umefanya, ama kile kilichokuleta hapa, ama—ama chochote kile, hilo lingeongeza imani yako, sivyo?

195 Ingeongeza yenu huko nje? Wakati, huu hapa mkono wangu; nijuavyo mimi, kamwe sijapata kumwona mwanamke huyu maishani mwangu, ni wachache tu kwenye kusanyiko, ama—ama labda alikuwa kwenye mstari wa maombi, ama kitu kama hicho, miaka na miaka iliyopita. Kumbukumbu lolote juu yake; la. Lakini Bwana na anisaidie sasa. Kama karama . . .

196 Mnaona, kama hawa wahudumu hapa. Tayari mnajua, kama mmenisikia nikihubiri, mimi—mimi si mhubiri. Sina elimu yoyote. Nisingeweza kujiita mhubiri, bali yupo mtu hapa ambaye anaweza hata na zaidi kufanya hivyo kuliko ninavyoweza mimi.

197 Lakini karama yangu inatoka kwa Mungu, maana ninampenda. Na—nami ninaamini hili, "karama na miito havina majuto." Zimekusudiwa tangu zamani na Mungu. Ziko katika kila kizazi. Na sehemu yangu katika huu ilikuwa ni kwa Neno

hilo, lipate kuishi tena, liwe Neno la kutambua na kujua. Hilo ni la kinabii, ambalo limeahidiwa kulingana na Malaki 4, kuwako katika siku hii, linatufanya kuwa katika siku ya mwisho kikamilifu.

198 Sasa kama Bwana Yesu akiniambia mahali shida yako ilipo, je! utaniamini mimi kwamba ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Na alijalie. Una ugonjwa wa ngo—ngozi. Ngozi yako ina kasoro fulani. Hiyo ni kweli. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Sasa kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Kwa hiyo . . .

199 Sasa ninaendelea kuhisi hilo likija kutoka huko nje, mtu fulani alisema, "Yeye alibahatisha hilo." Sasa hebu kidogo. Sikubahatisha hilo, mama. Baadhi, mnaona, wao . . . Huwezi kuficha wazo sasa, unaona, maana Yeye yupo hapa sasa. Nami ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, mnaona, kwa utukufu wa Mungu. Sikubahatisha hilo.

200 Huo ni ugonjwa wa neva. Una ugonjwa wa neva ambao unaninii . . . unaokusumbua. Unamwombea mpendwa. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Huyo ni mwanamke. ["Ndiyo."] Huyo ni mkaza mwanao. ["Ndiyo."] Naye ana ugonjwa wa kifafa. ["Naam."] Hiyo ni kweli.

Sasa sikubahatisha hilo. Vema.

201 Amini tu! [Huyo dada anasema, "Je! ameponywa?"—Mh.] Wewe amini kwa moyo wako wote; na kama unavyoamini, ndivyo itakavyokuwa kwako. Ninaamini. ["Ati ameponywa?"] Ni—nitaamini hilo. Kama wewe utaliamini, itakuwa hivyo.

202 Unaona, hawezi kuponywa kwa imani yangu, hana budi kuponywa kwa imani yake. Unaona? Unaona? Unafahamu.

203 U hali gani? Ndio kwanza nimpoteze mama yangu, karibu miaka miwili iliyopita. Nami ninapokuona ukikwea kuja huku jinsi hiyo, inanikumbusha. Hivi si ningekuwa ni mtu mbaya sana nikisimama hapa, nikimwakilisha Yesu Kristo, na niwe mdanganyifu? Hilo lingekuwa ni jambo baya sana kwangu kufanya ki—kitu kama hicho. Lakini mimi—mimi si mdanganyifu. Mimi ni mtumishi Wake. Na kama Mungu ataniruhusu, kwa neema Yake, kujua jambo fulani kukuhusu wewe, vema, utaamini ya kwamba linatoka kwa Mungu? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."]

204 Sasa kusudi watu wafahamu. Angalieni hapa, mnaona. Utambuzi huo mmoja ulikuwa ni zaidi kuliko kama ningelihubiri mpaka usiku wa manane. Yesu alisema, "Naona nguvu zimenitoka." Kama hiyo ilikuwa hivyo kwa Mwana wa Mungu, ni zaidi sana vipi kwangu mimi mwenye dhambi? Mnaona? Danieli aliona ono moja, akafadhaika kichwani mwake siku nyingi. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika. Mnaona? Hamtambui neema ambayo Mungu hutujalia.

205 Sasa, mama huyu ana ugonjwa wa tumbo. Ni tumbo lako. Ninakuona ukiondoka mezani. Na umesababishwa na u—ugonjwa wa neva unaolifanya tumbo liwe hivyo, ambao unafanya chakula kisimeng'enyuke. Ni vidonda vya tumboni, ndivyo hasa, tumboni. Nawe unaamini Mungu atakuponya huo? [Dada anasema, "Ninaamini."—Mh.] Unakubali kwamba umeponywa? Wewe amini kwamba Mungu atakuondolea huo. Mungu akubariki. Nenda, na Bwana Mungu na akujalie.

Iweni na kicho sana.

206 U hali gani? Sisi hatufahamiani, nadhani. Wakati wetu wa kwanza hasa kukutana, sivyo? [Huyo dada anasema, "Nimekuwa mikutanoni."—Mh.] Umekuwa mikutanoni. Bali mimi kukufahamu, sikufahamu.

207 [Ndugu Branham anatulia, kisha anawageukia wasikilizaji—Mh.] Ulikuwa ukijiuliza. Kama utaamini, hiyo yabisi kavu itakuacha. Naam. Yeye alikuwa ameketi pale, ameinamisha kichwa chake, akiomba. Itakuacha, kama utaamini. Mume wako, je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yake ni nini? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia? Ulikuwa na furaha sana kujua ya kwamba ataponywa huo. Una ugonjwa wa tezi kibofu inayokusumbua. Inua mkono wako.

208 Sijapata kuwaona, maishani mwangu. Hebu niambieni waligusa kitu gani. Sasa hebu ulizeni tu swali hilo. Waligusa nini? Kamwe hawakunigusa; wako futi thelathini kutoka kwangu. Lakini walimgusa yule Kuhani Mkuu.

209 Kama mimi ni mgeni kwenu enyi watu, punga mkono wako namna *hii*. Ninyi—ninyi—ninyi watu wawili mnaoketi hapa, kama mimi. . .Punga tu mkono wako namna *hii*, kama hatufahamiani. Mnaona? Mnaona? Mlikuwa mmeketi pale tu. Naye mama huyo alikuwa akiomba, mnaona; na Yeye, akisimama hapa, akageuka kama tu alivyofanya katika Biblia. Si—si mimi nikigeuka; Yeye akinigeuza.

210 Angalieni, siyajui mambo hayo. Ni kama tu maikrofoni hii, ni bubu kabisa bila kitu kuzungumza kuipitia. Lakini mnaweza kunisikia kupitia maikrofoni hii, (hiyo ni kweli?) bali maikrofoni haiwezi kuzungumza, yenyewe. Haina sauti. Siwajui watu hao. Hivi hamwezi kutambua ni katika Uwepo wa Mungu, anayeitumia hiyo, kuwaonyesha Uwepo Wake? Jipenyezeni moja kwa moja!

211 Sasa kwa kuwa hatufahamiani, wewe una umri mdogo kuliko wangu. Labda tulizaliwa tukiachana kwa miaka mingi na umbali wa maili kadhaa, na sisi hapa tukikutana kwa mara ya kwanza. Sasa wakati Hiyo ilipoenda huko, ninaweza tu kwenda; Ni Nuru, ninaiangalia, mnaona. Roho Mtakatifu ni Nuru, tunajua jambo hilo. Lakini kama Bwana Yesu atanisaidia kujua shida yako ni gani, utaamini kwamba mimi ni mtumishi Wake, na ujue kwamba sio mimi, kwamba ni Yeye?

212 Mimi ni mtumishi Wake tu, kama maikrofoni hiyo. Sasa, hili, dawati hili hapa ni sehemu ya fenicha za nyumba hii, bali halikutengenezwa lipate kuzungumza; linaishikilia Biblia yangu. Maikrofoni haitashikilia Biblia yangu; inaibeba sauti yangu. Vema, kuna karama mbalimbali kanisani; zingine ni sauti Yake, zingine ni ono, zingine ni mambo mengine zinazofanya. Lakini mimi ni kwa ono tu, kama mtumishi Wake.

213 Sasa kama Mungu atanijalia kujua shida yako ni gani, kile kilichokuleta hapa, utaniamini, na kuamini ya kwamba ni Neno la Mungu. Una ugonjwa wa kuambukiza. Ambukizo hilo liko kwenye ngozi. [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.]

214 Mnaona jambo hilo? Yeye anajua kama ni kweli ama si kweli. Mnaona? Sasa, kadiri ungeweza kuzungumza naye, ndivyo mengi yangeweza kusemwa. Yeye ni mtu mzuri sana.

215 Jambo lingine, hebu angalia hapa kwa dakika moja; halafu hao wengine, kama itawabidi kuwaleta haraka kidogo. Hebu tuzungumze tu dakika chache, kwa kuwa wewe ni mtu mzuri sana. Sasa unajua ya kwamba jambo fulani limetukia kwako. Sasa kati yako na mimi ipo Nuru. Ulipata kuona picha Yake? Inasimama papa hapa katikati yangu na wewe. Ninakuangalia, kupitia kwenye Nuru hiyo. Unaona? Nawe unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? Yeye alimwambia Simoni kwamba alikuwa ni nani.

216 Ni wangapi wanaoamini hilo sasa? Sisi hawa hapa tumeinua mikono yetu, hatufahamiani kabisa.

217 Wanakuita "Florence," na jina lako la mwisho ni McAllister. [Huyo dada anasema, "Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli."—Mh.] Unaamini Mungu anaweza kuniambia mahali unapotoka? ["Ndiyo."] Hutoki hapa. ["La."] Unatoka mahali panapoitwa Lawrence, Kansas. ["Hiyo ni kweli."] Hiyo ni kweli. Sasa rudi, Yesu anakufanya mzima. Um-hum.

218 Mwaminini Mungu. Mnaona? Mnaona nini? Sasa tafadhalini iweni na kicho. Msisogee. Mnaona, msisogee.

219 Mungu huponya kisukari. Unaamini hilo? Unaamini angekuponya? Endelea tu, na useme, "Asante, Bwana." Na uamini hilo kwa moyo wako wote, nawe utaponywa.

220 Unaamini Mungu anaweza kukuponya shida hiyo ya akina mama uliyo nayo? Basi nenda zako tu, ukisema, "Asante, Bwana. Ninaamini kwa moyo wangu wote."

221 Vema, acha mama huyo aje. Una shida ya akina mama, na pia una kisukari. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana," na uamini hilo kwa moyo wako wote sasa.

222 Njoo. Ugonjwa wa wasiwasi husababisha ugonjwa wa tumbo. Unaamini ungeweza kula chakula chako cha jioni sasa?

Nenda, ukisema, “Asante, Bwana.” Kula chakula chako cha jioni na uamini kwa moyo wako wote.

223 Mungu huponya ugonjwa wa moyo. Unaamini atauponya ugonjwa wako wa moyo? Vema. Nenda, ukiamini, naye atakuponya, unaona, kama ukiamini.

224 Vipi kama sikukwambia kitu chochote, kuonyesha tu imani ambayo ninaamini unayo, nikuwekee mikono tu, unaamini ungepona? Pitia hapa. Ulikuwa tayari umeponywa wakati ulipoondoka pale juu, na huo. Ni kweli kwa vyovyote vile.

225 Njoo. Hakika, kila mtu anaona mwanamke huyu anachechemea, huku kumekuwa ni maishani mwake mwote. Lakini jambo lingine ulilo nalo, ni ugonjwa wa tumbo unaokusumbua, ambao unataka...Endelea tu kutembea, ukisema, “Asante, Bwana.” Amini kwa moyo wako wote, na uende, na uamini.

226 Unaamini Mungu ataponya hiyo yabisi kavu, na kukupa afya, nawe uende nyumbani? Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote.

227 Ni wangapi huko nje wanaamini, ninyi nyote? Huyu hapa mtu ameketi hapa akiniangalia hapa. Hivi hamwioni ile Nuru ikining’inia juu ya mtu huyu papa hapa?

228 Kweli, kile kinachomsumbua, kinahusu uzito wa kupita kiasi. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako kama ndio. Unaamini Mungu atakuponya? Mke wako ameketi hapo karibu nawe, unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Unaamini? Utaamini, ewe mama? Unaamini mimi ni nabii Wake, mtumishi Wake? Hilo huwapofusha watu unaposema “nabii.” Unaamini mimi ni mtumishi Wake? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Presha ya juu ya damu. Amini kwa moyo wako wote sasa, nao utakuacha, maana unaamini.

229 Mvulana huyu mweusi anayeketi hapa mwishoni mwa kiti, akiangalia kwa makini, unawazia nini juu ya jambo hili, bwana? Unaamini kwamba ni la Mungu, wewe unayeketi hapo? Ulikuwa ukiniangalia kwa makini sana. Sikujui. Hatufahamiani. Lakini unaugua ugonjwa fulani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba ni upi? Unaamini? Ni mzio. Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Jambo moja kuu kukuhusu wewe, ni hili, shida yako moja kuu sana ni kwamba umerudi nyuma. Kweli unataka kumrudia Mungu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, kisha uje hapa. [Ndugu huyo anasimama na kuja mbele—Mh.] Dhambi zako zimesamehewa, ndugu yangu.

230 Unasema, “Unajuaje hilo?” Yeye yule aliyeniambia shida yake ilikuwa ni nini.

231 Ni wangapi walio hapa ndani wanaotaka dhambi zao zisamehewe? Mtasimama kwa miguu yenu? Mnataka dhambi zenu zisamehewe? Ninataka tu kuona kama ninyi ni waaminifu

vya kutosha kufanya hivyo. Asanteni. Sijui kama mngeweza kuja papa hapa na kusimama hapa pamoja na mtu huyu ambaye ndiyo kwanza asamehewe, mseme, "Ninataka dhambi zangu zisamehewe. Mimi ni mwaminifu juu ya jambo hilo"? Huwezi . . .

232 Njoo huku, kuna wengi kuliko hao hapa. Sasa, kama utambuzi hutambua maradhi na magonjwa, unaitambua dhambi. Mnajua hilo. Ningejuaje mtu huyu alikuwa ni mwenye dhambi? Jambo ndilo hilo, tokeni mje hapa na kusimama papa hapa chini. Tuninii tu . . . Mtafanya hivyo, kwa dakika moja tu? Njoni hapa mkasimame kwa dakika moja, mseme, "Ninataka kusamehewa, ndugu. Ninataka Mungu anisamehe makosa yangu. Ninatambua ya kwamba niko katika Uwepo Wake. Sijali majirani wangu wanawazia nini. Na—naja kwa vyovyote vile. Mimi ni mng'ang'anizi. Ninataka kuokolewa, usiku wa leo. Ninamwamini Mungu. Ninataka kuja sasa hivi na kuoshwa dhambi zangu zote."

233 Je! ni sawa kuwaita wahudumu? Ni wahudumu wangapi walio humu ndani, ambao wanaamini ya kwamba watu hawa wana haki ya kuokolewa kwa neema ya Mungu? Ninamtaka kila mhudumu anayeamini hilo, aje asimame hapa pamoja nao wakati tukiomba, kila mhudumu anayevutiwa na nafsi zilizopotea. Sikudhani nilikuwa nifanye hivi, bali ninajua vizuri zaidi kuliko kuiasi Sauti Yake. Yeye aliniambia nifanye hivi. Huenda ikawa ndio wakati wao wa mwisho, sijui mimi.

234 Ni wangapi wanaojua ya kwamba hivi ndivyo alivyofanya wakati alipokuwa hapa duniani? Basi haina budi kuwa ni Yeye tena. Haiwezekani kwa mwanadamu, mwanadamu yeyote, kufanya kitu kama hicho. Tuko katika Uwepo Wake. Na hapa tunamwona, usiku wa leo, akifanya . . . "Kama nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu." Mnaona? Tunamwona hapa akifanya jambo lile lile alilofanya wakati alipokuwa hapa duniani. Hivi hatuwezi kuwa wang'ang'anizi sasa? Penyezeni mwingie. Ni kitu gani kilichotufanya kuja hapa? Ni kitu gani kilisababisha yote haya, kwa vyovyote vile? Ni Mungu. Hivi hamwamini hilo?

235 Ninawataka kila mmoja wenu ndugu wahudumu kuja mbele na kuweka mikono yenu juu ya mmoja wa hao watu wanaokiri pale.

236 Sasa, ndugu yangu mpendwa, dada, ninyi ambao mnakiri madhababuni, ni kitu gani kilichowafanya kuja? Hamkuja kwa nguvu zenu wenyewe. Mlikuja kwa sababu kitu fulani kiliwashawishi kwamba mlikuwa mmekosea. Mnataka kusamehewa. Wakati mlipomwona maskini yule mvulana mweusi, yule mvulana Mwethiopia amesimama pale, aliyemwacha Mungu, Naye Roho Mtakatifu akafunua ya kwamba yeye alikuwa ni mwenye dhambi. Roho Mtakatifu yuyo huyo kamwe hakukuita moja kwa moja kutoka midomoni

mwangu, bali alikuita, nawe huyu hapa, usiku wa leo, umesimama vile alivyosimama yule mvulana. Kiri dhambi zako sasa mbele za Mungu. Mwamini kwa moyo wako wote, Naye ataisamehe kila dhambi uliyotenda, na kukurejesha usiku wa leo kwa msingi wa imani yako na ushirika. Atafanya hayo kama tu utamwamini.

237 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu, kila mahali kwenye wasikilizaji, na kila mtu awe na kicho kabisa. Sasa na tuombe. Kila mmoja wenu na utubu dhambi zako. Yeye yupo hapa. Roho Mtakatifu yupo hapa. Huyo ndiye anayeita. Sasa amini tu kwa moyo wako wote, kiri kwamba umekosea, mwombe akusamehe. Na kila mmoja wenu ndugu omba pamoja na watu hawa.

238 Baba wa Mbinguni, tunakuja sasa katika Jina la Bwana Yesu, tukikushukuru kwa ajili ya neema Yako kuu na nguvu kwa ajili yetu, Bwana. Kwamba sisi, tusiostahili, huku chini kabisa katika wakati huu uliochelewa, wa kufunga. Tunaomba ya kwamba rehema yako ienee, Bwana, ishuke, mpaka nafsi ya mwisho itakapoingizwa. Usiku wa leo, kwa sababu ya kuonekana Kwako mbele zetu, iliwafanya watu wasukume kupitia kila hali ya mambo, kupanda hapa juu, kuamini ya kwamba hii ndiyo saa ambayo dhambi zao zitasamehewa, na kwamba watakuwa huru, tangu usiku huu na kuendelea. Tujalie, Baba wa Mbinguni. Jalia kila dhambi iwaondokee.

239 Ulisema, "Yeye anijiaye Mimi sitamtupa nje kamwe. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama sufu; nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama theluji." Tunajitumbukiza chini ya mafuriko ya Damu ya Yesu Kristo. Kwa imani tunawapeleka watu hawa, wanaokiri, katika Uwepo wa Mungu, waingie katika Damu ya Mwana wa Mungu, na kuomba msamaha kwa ajili yao. Tunaomba dua hili katika Jina la Yesu. Ondoa kila dhambi na uwachukue katika ulinzi Wako, Baba. Wanapokiri, warejeshe juu ya msingi wa ahadi Yako. Ulisema ungefanya hivyo, nami ninajua utafanya. Hao ni Wako, Baba. Tunawatoa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

240 Kila mmoja wenu anayesimama kuizunguka madhabahu sasa, ambao kweli mmekiri kwamba mmekosea; na mko katika Uwepo wa Mungu, mnaamimi Mimi ni nabii Wake, na mnaamini ya kwamba nimewaambia Ukweli juu ya hili, na mnaamini ya kwamba dhambi zenu zimeondoka; nanyi sasa, kwa imani, mmepasua mkapitia kwenye lile pazia, mkaingia katika Uwepo wa Mungu, na kusema, "Bwana, ninakuamini Wewe sasa hivi, na kukukubali"? Inueni mikono yenu, na kusema, "Ninaamini." Kila mmoja kuizunguka madhabahu, inueni mikono yenu na kusema, "Ninafanya hivyo. Sasa ninaamini hilo." Mungu awabariki. Amina. Hiyo ndiyo njia ya kufanya hivyo. Haya basi. Kwa imani tu, pasua upitie kwenye pazia hilo.

241 Sasa wakati mkiwa kwenye maeneo yale yale mnayosimama, kwamba mmesamehewa, sasa, ndugu, wekeni mikono yenu juu yao tena kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mahali pale pale mnaposimama, wawekeeni mikono yenu sasa, na muombe ya kwamba waupokee ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakisimama papa hapa.

242 Bwana Yesu, tuma nguvu Zako juu yao, kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Tuma marudio mengine ya Pentekoste; na uwajaze watu, si chumba, watu, kwa Moto wa Roho Mtakatifu, na msamaha, na madhihirisho ya nguvu, kupitia kwa Jina la Yesu. Amina.

Anayeng'ang'ania SWA64-0619
(Perseverant)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 19 Juni, 1964, katika Ukumbi wa Manispaa huko Topeka, Kansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org